# MITAZAMO YA VIJANA NA WAZEE KUHUSU UKOMBOZI WA MWANAMKE KATIKA TAMTHILIA TATU ZA KISWAHILI

NA

JOHN M. MUTUA

TASNIFU HII IMETOLEWA ILI

KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA

YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI

University of NAIROBI Library

0472326 8

JUNI 2007

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa kutosheleza mahitaji ya shahada ya uzamili katika chuo kingine chochote.

.......................................... 6/11/2007 ..........................................

**John Musyoka Mutua** **Tarehe**

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi.

.......................................... 6/11/07 ..........................................

**Dkt. Kineene wa Mutiso** **Tarehe**

.......................................... 6th NOV 2007 ..........................................

**Dkt. Rayya Timammy** **Tarehe**

## KUTABARUKU

Natabaruku na wazazi wangu. Mama Susan Katumbi kwa kunizaa, kunilea na kunisomesha. Baba Jonathan Mutua kwa maazimio yake aliyokuwa nayo juu yangu ambayo yalikatizwa na mkono wa kifo.

# SHUKRANI

Tasnifu hii haingeweza kukamilika bila usaidizi, uongozi na mchango wa watu wengi. Ni vigumu kuwataja wote. Hata hivyo, nitawataja wachache.

Ningependa kutoa shukrani maalum kwa Dkt. Kineene wa Mutiso kwa mawaidha na ushauri wake wa busara, mwongozo na masahihisho aliyonipatia wakati nilipokuwa katika hali ya kutojua ni njia ipi nitakayoifuata katika bahari hii ya usomi na utafiti. Kama msimamizi wangu, hakuchoka kuisoma kazi yangu kila nilipompelekea na kunishauri ipasavyo. Mungu amzidishie baraka.

Shukrani za dhati pia nazitoa kwa Dkt. Rayya Timammy ambaye alipitia sehemu mbalimbali za kazi yangu kwa haraka na kwa umakini na kuniwezesha kuukamilisha utafiti wangu kwa muda mfupi. Mawaidha yake mema yalinitia ari na mshawasha wa kuwaza zaidi na kuandika kazi bora. Mola azidi kumpa hekima na neema.

Kwenu Prof. Kithaka wa Mberia, Dkt. E.M Mbuthia na Prof. Geoffry Kitula King'ei (Chuo Kikuu cha Kenyatta) nasema ahsanteni kwa jinsi mlivyonielekeza na kunipa mwangaza na ushauri juu ya masuala muhimu kuhusiana na mada ya kazi yangu. Mola awabariki.

Shukrani za dhati pia nazitoa kwa wahadhiri wangu katika idara ya isimu na lugha ya Chuo Kikuu cha Nairobi walionisaidia, kuniongoza na kunielekeza katika safari hii ya usomi ambayo haikuwa rahisi. Hawa ni, Prof. Mohammed H. Abdulaziz, Dk. K. W. Wamitila, Prof. Lucia Omondi, Dkt. Tom Olali, Dkt. John Habwe,Dkt. Zaja Omboga, Dkt. Mwenda Mbatiah ( Mwenyekiti wa idara ya isimu na lugha).

Sitasahau kumshukuru mratibu wa shughuli za usimamizi wa wanafunzi Dkt. Jayne Mutiga kwa kuongoza na kusimamia shughuli za kuwasilisha mapendekezo ya utafiti wa wakufunzi wa mwaka wetu kwa njia ya busara na ukomavu.

Kwa wakufunzi wenzangu ambao tulishirikiana katika safari hii ya kutafuta shahada ya uzamili, mabwana Gerald Mogere, Samson Ongarora, Henry Njoroge, Enock Matundura na Evans Ogoro. Wenzetu katika isimu ni Were, Unice Jebet, Ann Ndunge, Violet Aura, Jacline, na Ann Obinju. Nawaombea dua njema wafanikiwe katika kila watendalo. Pia nawia shukrani wenzetu waliotutangulia katika mwaka wa pili hasa nikiwakumbuka Bw. Jacktone Nyonje, Bw. Samuel Ng'ang'a, Bi. Esther Muli na Bi. Elizabeth Katola.

Shukrani za dhati ya moyo wangu ni kwa mke wangu mpenzi Bi. Magdalena Ngina. Wema wake, usaidizi na uvumilivu wake ndio ulioniwezesha kuianza, kuiendeleza na kuitimiza safari hii. kwa watoto wetu, Kennedy Wambua na Juliet Ndanu nasema ahsanteni kwa kunivumilia, kunielewa na kunitakia ufanisi.

Namsheheneshea shukrani tele Bw. Moses Muindi kwa kunifaa kwa hali na mali nilipokuwa katika matatizo makubwa ya kifedha. Vivyo hivyo, namshukuru ndugu yangu Bw. Paul Maundu pamoja na wakwe zangu, John Mwangani na Betrice Kavesu kwa msaada wao usio adimu. Sitamsahau Bw. Peter Mbuna kwa kunihimiza siku zote nilipoelekea kukata tamaa. Nyote Mungu awazidishie baraka.

Mwisho namtolea shukrani Bi. Catherine Muindi kwa kujitolea kuipiga chapa tasnifu hii.

# MUHTASARI

Madhumuni ya utafiti huu yalikuwa ni kushughulikia swala la mitazamo ya vijana na wazee kuhusu ukombozi wa mwanamke katika tamthilia tatu za Kiswahili. Tamthilia zilizoteuliwa ni: *Kitumbua kimeingia mchanga* (2000) S. Mohamed, *Migogoro* (2006) M. Mbatiah na *Natala* (1997) K. wa Mberia. Pamoja na kazi hizi pia tulipitia kazi mbalimbali zilizohusiana na mada ya utafiti ili kujifahamisha na maswala yanayohusu wanawake.

Sura ya kwanza ni usuli wa utafiti ambapo somo la utafiti, madhumuni, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka ya utafiti pamoja na nadharia tete zimeshughulikiwa. Aidha, msingi wa nadharia, yaliyoandikwa kuhusu somo hili pamoja na njia za utafiti zimeangaziwa.

Sura ya pili inachunguza namna mbalimbali ambavyo wanawake wanadhulumiwa kwa mujibu wa kazi hizi tatu. Vile vile, tumejadili baadhi ya juhudi zinazofanywa ili kumkomboa mwanamke. Pamoja na hayo, tunamulika baadhi ya changamoto zinazozikabili harakati za kumkomboa mwanamke.

Katika sura ya tatu tunajihusisha na mitazamo ya vijana wa kike na wa kiume kuhusu ukombozi wa mwanamke. Aidha, tunachunguza baadhi ya sababu zinazowapelekea vijana kuwa na mitazamo hiyo.

Sura ya nne inashughulikia mitazamo ya wazee wa kike na wa kiume kuhusu swala la ukombozi wa mwanamke. Vile vile, sababu za wazee kuwa na mitazamo hiyo zinachunguzwa. Mwisho, tunalinganisha mitazamo ya vijana na wazee.

Katika sura ya tano tunatoa muhtasari wa matokeo ya utafiti pamoja na mapendekezo kuhusu tafiti za baadaye.

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | | |
|---|---|---|
| Bi. | - | Bibi |
| Bw. | - | Bwana |
| Dkt. | - | Daktari |
| Prof. | - | Profesa |
| Uk. | - | Ukurasa |
| N.k. | - | Na kadhalika |
| Ba. | - | Baba |

## YALIOMO


Mada .................................................................... (i)

Ungamo .................................................................... (ii)

Kutabaruku .................................................................... (iii)

Shukrani.................................................................... (iv)

Muhtasari .................................................................... (vi)

Orodha ya vifupisho .................................................................... (viii)

Yaliomo .................................................................... (ix)

SURA YA KWANZA

1.0. Utangulizi .................................................................... 1

1.1. Tatizo la utafiti .................................................................... 2

1.2. Madhumuni ya tasnifu .................................................................... 2

1.3. Sababu za kuchagua mada .................................................................... 3

1.4. Upeo na mipaka ya tasnifu .................................................................... 4

1.5. Yaliyoandikwa kuhusu mada.................................................................... 5

1.6. Msingi wa kinadharia .................................................................... 8

1.7. Nadharia tete .................................................................... 10

1.8. Njia za utafiti .................................................................... 10

SURA YA PILI

NAMNA MBALIMBALI AMBAVYO WANAWAKE WANADHULUMIWA

2.1.0 Utangulizi .................................................................... 12

2.1.1 Kuachishwa shule na kuozwa .................................................................... 12

2.1.2 Kudharauliwa na kitukaniwa ukoo wake .................................................................... 13

2.1.3 Kulimbikiziwa kazi za jikoni na kuhusishwa na watoto wajeuri .......... 15

2.1.4 Kunyimwa uhuru wa kujichagulia mchumba....................................16
2.1.5 Kutokubaliwa kujiunga na siasa.............................................17
2.1.6 Kupigwa na kuthibitiwa........................................................17
2.1.7 kudhulumiwa kimapenzi na kunyimwa uhuru...............................18
2.1.8 Mila zinazohimiza kurithi wajane...............................................19
2.1.9 Umaskini.........................................................................20
**2.2.0 JUHUDI ZINAZOFANYWA KUMKOMBOA MWANAMKE...........................21**
2.1.1 Wanawake kushirikiana na wanaume............................................21
2.2.2 Kujiendeleza kimasomo na kutotia matumaini katika ndoa..................23
2.2.3 Kufuata mifano ya wanawake waliojikomboa...................................24
2.2.4 Kuanzisha miradi ya kujisaidia..................................................24
2.2.5 Serikali kutoa ufadhili kwa wanafunzi bora...................................25
2.2.6 Kupuuzilia mbali tamaduni kandamizi..........................................26
**2.3.0 CHANGAMOTO ZINAZOZIKABILI JUHUDI ZA KUMKOMBOA MWANAMKE ..........................................................................................27**
2.3.1 Uhafidhina wa wazee............................................................27
2.3.2 Kuvunjwa moyo na wanaume....................................................28
2.3.3 Ukosefu wa elimu kwa viongozi wa wanawake...............................29
2.3.4 Kutopewa uhuru wa kuchagua maisha..........................................30
2.3.5 Ukosefu wa mtaji..................................................................30
2.3.6 Hitimisho .........................................................................31

**SURA YA TATU**

**MITAZAMO YA VIJANA KUHUSU UKOMBOZI WA MWANAMKE**

3.1.0 Utangulizi.........................................................................33
3.1.1 Kusoma na kupata kazi nzuri....................................................33
3.1.2 Kufa au kubadilika kwa mila zinazomgandamiza mwanamke................34
3.1.3 Kupinga kuchaguliwa wachumba na kuozwa mapema........................34

3.1.4 Kukuza uhusiano mwema baina ya wanawake na wanaume ..........................35
3.1.5 Wanawake kuungana kutetea maslahi yao ..................................................36
3.1.6 Vijana kuwa msatari wa mbele kutetea wanawake.......................................36
3.1.7 Wanawake wadai uhuru wao ........................................................................37
3.2.0 MTAZAMO WA VIJANA WA KIUME KUHUSU UKOMBOZI WA WANAWAKE..........38
3.2.1 Kuwaunga mkono wanawake katika juhudi zao .........................................39
3.2.2 Kukosa msimamo thabiti ..............................................................................39
3.3.0 SABABU ZA VIJANA KUWA NA MITAZAMO HIYO............................................40
3.3.1 Elimu na ajira ni nguzo muhimu katika ukombozi ......................................41
3.3.2 Mila za kale zimepitwa na wakati ..................................................................41
3.3.3 Haja ya kubadilika na wakati .........................................................................41
3.3.4 Tathmini.........................................................................................................42
3.3.5 Hitimisho........................................................................................................44

SURA YA NNE

MITAZAMO YA WAZEE WA KIKE NA WA KIUME KUHUSU UKOMBOZI WA MWANAMKE

4.1.0 MITAZAMO YA WAZEE WA KIKE.................................................................46
4.1.1 Utangulizi .....................................................................................................46
4.1.2 Mwanamke anastahili kudhibitiwa tangu utotoni .........................................46
4.1.3 Mahali pa mwanamke ni jikoni .....................................................................47
4.1.4 Kuwadharau na kuwaumbua binti zao ..........................................................47
4.1.5 Lazima mila kuheshimiwa .............................................................................48
4.1.6 Uhuru wa kuvaa .............................................................................................49
4.1.7 Taasubi ya kiume ...........................................................................................50

**4.2.0 MTAZAMO WA WAZEE WA KIUME ............................ 51**

4.2.1 Utukufu wa nasaba na uchumi ........................................ 51

4.2.2 Lazima mila kudumishwa ........................................ 52

4.2.3 Haja ya kuwaelewa vijana ........................................ 52

4.2.4 Kuheshimu haki na uhuru wa vijana........................................ 53

**4.3.0 SABABU ZA KUWA NA MITAZAMO HIYO.................... 54**

4.3.1 Jukumu la kulinda mila na desturi za kale ............................ 54

4.3.2 Wanawake na siasa ........................................ 55

4.3.3 Elimu kama msingi wa ukombozi........................................ 56

**4.4.0 KULINGANISHA MITAZAMO YA VIJANA NA WAZEE ...... 57**

4.4.1 Hitimisho........................................ 59

## SURA YA TANO

## HITIMISHO

5.0 Utangulizi ........................................ 62

5.1 Muhtasari wa matokeo ya utafiti ........................................ 62

5.2 Tafiti za baadaye ........................................ 67

5.3 Marejeleo........................................ 68

# SURA YA KWANZA

## USULI WA TASNIFU

### 1.0 Utangulizi

Katika utafiti huu istilahi 'drama' na 'tamthilia' zimetumika. Ingawa tunatambua tofauti finyu katika istilahi hizi mbili, tumezitumia kwa maana sawa. Vile vile, neno mwanamke limetumiwa kumaanisha wanawake. Aidha, nene 'mitazamo' limetumiwa kumaanisha namna ambavyo mtu anavyolichukulia jambo.

Suala la ukombozi wa mwanamke limewashughulisha wataalamu wa fasihi ya Kiswahili kwa muda mrefu sana. Pengine umuhimu wake unatokana na majukumu mengi yanayotekelezwa na mwanamke katika Jamii. Kazi nyingi za kifasihi kama zile za A. K. Katini, *Mama Ee* (2003) na A. Mazrui, *Kilio cha Haki* (1982) tulizozisoma zimemchora mwanamke kama mhusika au kiumbe aliyedharauliwa.

Tafiti nyingi zilizofanywa katika fasihi ya Kiswahili zinadhihirisha mtazamo hasi kuhusu jinsia ya kike. Hata hivyo, zipo nyingine zinazomsawiri mwanamke kwa njia chanya.

Baadhi ya wahakiki tuliosoma kazi zao wamejishughulisha na utafiti kubainisha namna mbalimbali ambavyo wanawake wamedhulumiwa na tamaduni ambazo zinaegemea mawazo ya kiubabe-ume. Tafiti hizo zimebainisha baadhi ya sababu zinazowafanya wanawake kutwezwa pamoja na kuibusha mikakakati ambayo imebuniwa na wanawake hao kujitetea. Jambo la kutushangaza ni kuwa, hata baada ya kutambua changamoto chungu nzima zinazozikabili juhudi zao za kujinusuru, hakujatokea mhakiki hata mmoja aliyeazimia kuduhusa namna jamii nzima inavyolipokea suala zima la ukombozi wa mwanamke, kama anavyosema C.Momanyi (2002);

> Pengine suala la uana na mapambano ya kiitikadi dhidi ya ugandamizwaji wa wanawake halijapokelewa vyema miongoni mwa jamii za kiafrika kutokana na dhana kuwa harakati hizo ni za kimagharibi (uk.24).

Utafiti wetu umejikita kwenye tamthilia teule za Kiswahili kwa kutambua namna ambavyo sanaa hii inavyoweza kusababisha mvuto na athari kubwa kwa hadhira yake. Vile vile, tumelenga vijana kwa imani kuwa wao ni wengi, wamesoma na wanakumbatia sana fikira za kimapinduzi na kimaendeleo kinyume na wazee ambao ni kielelezo cha uhafidhina na ukale.Tumeweza kubainisha namna vijana na wazee wanavyolichukulia swala la ukombozi wa mwanamke na tunaamini hiyo itakuwa ni hatua muhimu katika utatuzi wa kadhia hii.Tamthilia tulizohakiki ni; *Kitumbua kimeingia mchanga* (S. Mohamed ), *Migogoro* (M. Mbatiah ) na *Natala* (K. wa Mberia).

## 1.1 Tatizo la utafiti

Kwa muda mrefu, wanawake wamekuwa wakipigania haki na usawa pasipo mafanikio makubwa. Pengine mawazo haya ni ya kimagharibi na hayajapokelewa vyema miongoni mwa watu katika jamii za kiafrika. Labda tatizo hili linazidishwa na ukinzani wa kimtazamo baina ya vijana na wazee katika jamii kuhusu ukombozi wa mwanamke.

Kwa sababu hii, tunachunguza mitazamo ya vijana na wazee kuhusu ukombozi wa wanawake katika tamthilia tatu za Kiswahili zilizotajwa hapo juu.

## 1.2 Madhumuni ya tasnifu

(i) Kutathmini nafasi ya vijana katika ukombozi wa mwanamke.

(ii) Kuchunguza juhudi zinazofanywa na wazee kumtetea mwanamke dhidi ya asasi za jamii zinazomtweza.

(iii) Kubainisha jinsi mwanamke anavyokandamizwa na changamoto zinazozikabili juhudi za kumkomboa.

### 1.3 Sababu za kuchagua mada

Suala la ukombozi wa mwanamke ni muhimu kwa sababu ya utambuzi wa nafasi yake katika kuleta maendeleo katika jamii.

Kwa muda mrefu, wahakiki wengi wa masuala ya wanawake katika fasihi wamejikita katika kuchunguza usawiri wa mwanamke kwenye tanzu za riwaya na ushairi. Aidha, wametalii namna mbalimbali ambavyo wanawake wamedhulumiwa na mfumo mzima wa jamii za kiubabe-ume. Kutokana na hali hii basi, tunashawishika kujishughulisha na utafiti juu ya mtazamo wa jamii kuhusu ukombozi wa mwanamke katika tamthilia za Kiswahili.

Sababu nyingine ya kuchagua mada hii inatokana na imani yetu kwamba, mtazamo wa vijana na wazee kuhusu swala hili haujawahi kubainishwa katika utafiti wowote katika kazi tulizozipitia na hasa katika drama za Kiswahili.

Tumeteua mada hii kutokana na umuhimu wa suala linalohusika; sisi, kama wahakiki wa kazi za fasihi, tungependa kuendeleza uchambuzi wa wahakiki waliotutangulia kwa kuibua mtazamo wa jamii juu ya ukombozi wa mwanamke.

Pia, tunaamini ya kwamba, kutokana na sifa ya drama ya kuakisi, kuathiri na kuhaisha matendo halisi ya jamii husika, itatuwezesha kudhihirisha wazi migogoro inayosababishwa na tofauti za kimtazamo kuhusu mada inayotafitiwa.

Sababu nyingine ni kuwa, kwa kuwa sasa kuna harakati zinazoendelea za kupigania ukombozi, haki na usawa wa mwanamke katika jamii, uhakiki huu utakuwa nyenzo madhubuti ya kutolea mchango wetu katika harakati za kumkomboa mwanamke.

Kama alivyosema C. Ndungo (1985), ukombozi wa mwanamke hauwezi kupatikana pasipo jamii zima; wanawake kwa wanaume kushiriki.

Tamthilia zilizoteuliwa ni; *Kitumbua kimeingia mchanga,* (S. Mohamed), *Migogoro* (M.Mbatiah) na *Natala* (K. wa Mberia). Kazi hizi zinawakilisha vizuri mitazamo tofauti ya makundi mawili katika jamii ambayo ni vijana na wazee.

Sababu za kuchagua tamthilia hizi ni: kwanza, tamthilia hizi ni mpya na hazijahakikiwa kwa kina. Pili, zinaakisi mada yetu kwa njia inayofaa. Kwa mfano, mawazo ya kuhitilafiana baina ya vijana na wazee, kuhusu swala la wanawake yanadhihirika kwa njia ya wazi zaidi. Tatu, drama ni chombo muhimu katika kubadilisha mitazamo ya jamii kuhusu swala husika.

**1.4 Upeo na mipaka ya tasnifu**

Utafiti huu ni wa kifasihi na kwa hivyo uchunguzi wetu umejikita katika uhakiki wa tamthilia tatu ambazo ni; *Migogoro* ya M. Mbatiah (2006), *Kitumbua kimeingia mchanga* ya S. Mohamed (2000) na *Natala* ya K. wa Mberia (1997).

Uhakiki huu umejihusisha na mitazamo ya vijana na wazee kuhusu ukombozi wa mwanamke katika tamthilia zilizotajwa hapo juu. Aidha, tumeziteua kazi hizi kama sampuli kwa sababu ya ufinyu wa muda tuliotengewa kuukamilisha utafiti huu. Muda mfupi tulio nao hauturuhusu kushughulikia tamthilia zote zinazoangazia suala hili. Hata hivyo, tunatambua kuwepo kwa kazi nyingine zinazoangazia swala letu lakini tutajikita katika kazi tulizozitaja hapo juu. Hata hivyo, uteuzi huu hautunyimi fursa ya kugusia tamthilia zingine kama mifano ya kushadidia hoja zetu inapohitajika kufanya hivyo.

### 1.5 Yaliyoandikwa kuhusu mada

R. Lugano (1989) alishughulikia suala la wanawake kwa kuangalia jinsi wanavyoumbwa na kusawiriwa kisiasa, kiuchumi, kijamii na kielimu katika riwaya tatu za Kezilahabi. Anasema kuwa katika riwaya zote, hali ya mwanamke inakuwa ni ile ile ya kumtegemea mwanamume kiuchumi, kuwa chombo cha kumfurahisha mwanamume, chanzo cha maovu katika jamii n.k. Wanawake katika jamii yake hawafanyi chochote kupinga dhuluma inayowakabili.

Utafiti wake umeegemea kwenye riwaya za mwandishi mmoja 'Kezilahabi' tofauti na wetu ambao unachunguza kazi za waandishi watatu tofauti. Hata hivyo, utafiti wake umetunufaisha kwa kuwa unafichua taswira dumifu kuhusu hadhi ya mwanamke katika jamii. Sisi tunapania kudhihirisha mitazamo ya jamii kuhusu suala hili.

L. Dhahabu (1994) naye anachunguza uumbaji na uendelezaji wa wahusika katika tamthilia nne za Penina Muhando. Ingawa uhakiki wake unakabiliwa na ufinyu wa kuegemea mwandishi mmoja, kazi hii ni muhimu kwetu kwa kuwa inahakiki kipengele cha wahusika ambacho kwa mujibu wa utafiti wetu tumewagawa katika makundi mawili; vijana na wazee. Utafiti wake hautupi mwanga kamili kuhusiana na hisia za wahusika wake juu ya ukombozi dhidi ya dhuluma kwa wanawake, hata ingawa unadhihirisha taswira ya wahusika wanawake wanaonyanyaswa. Sisi tumepiga hatua mbele na kupeleleza jinsi jamii inavyochukulia ukombozi wao.

S. Kiango (1992) ameangazia taswira ya mwanamke katika tamthilia za Kiswahili za Kenya. Amesema kuwa mwanamke anaonyeshwa kama mtu asiye sawa na mwanamume na kuchorwa kama kitega uchumi, mbaya, mzinifu, mtoaji mimba na mtupaji watoto. Utafiti wake umetufaidi kwa kuwa unatilia mkazo kuwa wanawake wamedhulumiwa na wanahitaji ukombozi. Anapohakiki tamthilia ya *Kilio cha haki* (Alamin Mazrui), anadokeza kwamba tamthilia hii inastahili kupewa mtazamo mwingine kwa kuwa mkabala wake ni wa kimapinduzi, yaani analiangalia tatizo la

wanawake kwa njia chanya. Bali na kuwa anaunga mkono ukombozi wa mwanamke, utafiti wake haukupigia darubini jinsi ambavyo wahusika vijana na wazee wanavyolichukulia suala hilo. Utafiti wake unajishughulisha na utanzu wa riwaya na kwa hivyo ni tofauti na wetu, unaohakiki utanzu wa tamthilia.

H. Nyamberi (1997) naye alijishughulisha na 'mwamko wa wanawake katika tamthilia nne za Penina Muhando'. Alichunguza juhudi za mwanamke za kupigania uhuru wao kutokana na udhalimu wa kijamii, kisiasa na kiuchumi.

Utafiti wa Nyamberi umetufaa kwa kuwa unazingatia juhudi za mwanamke kujikomboa. Pia, unaangazia baadhi ya pingamizi zinazomkabili mwanamke katika harakati hizo. Hata hivyo, uchunguzi wake unatofautiana na wetu kwa kuwa; anachunguza kazi ya mwandishi mmoja na wetu unapanuka zaidi kwa kuwahakiki wasanii watatu tofauti. Isitoshe, suala letu ni la kimtazamo wa jamii kuhusu ukombozi wa mwanamke.

E. Mugambi (1982) Amehakiki tamthilia za Kiswahili za Kenya zilizochapishwa baina ya (1956-1982). Uhakiki wake unalenga ulinganifu wa kimaudhui kwa kutumia mtazamo wa u-marx. Utafiti wetu unahusu kazi zilizochapishwa karne ya ishirini na moja
(hivi juzi) na tutaongozwa na nadharia ya ufeministi wa kiharakati. Isitoshe, haujishughulishi na tamthilia nyingi kama wake. Ni wazi kuwa utafiti wake haungeweza kuwa wa kina, kwa sababu ya wingi wa kazi alizozishughulikia.

Ufaafu wa kazi yake kwetu unatokana na ile kauli aliyotoa alipokuwa akimnukuu Va'Squez (1965:24-25), anasema kwamba;

> "..........kwa vyo vyote vile ukombozi hauna budi
> upatikane na pia ukombozi huu utatokana na juhudi
> za jamii iliyokandamizwa kwa kuzipigania haki zake
> hata ikiwa mauti ni ya lazima. Anaongeza kuwa

> fasihi yetu nayo haina budi idhihirishe mtafaruku
> huu kwani yenyewe ni kielelezo cha hisia ambazo
> zategemea vile taratibu zilivyo katika maisha ya
> jamii (Tafsiri yetu).

K. Mogambi (1983) anahakiki hali ya wanyonge kama wanavyojitokeza katika riwaya tatu za S. Mohamed. Utafiti wake, ingawa unachunguza kazi ya mwandishi tunayemchunguza katika utanzu wa tamthilia, yeye anajishughulisha na riwaya zake. Anapodhihirisha sababu zinazochangia unyonge wao anaunufaisha utafiti wetu kwa kuwa, lengo letu ni kuduhusa maoni kuhusu ukombozi wa kundi moja linalochukuliwa kuwa 'nyonge' katika jamii.

C. Ndungo (1985) aliangalia jinsi wanawake walivyochorwa katika nyakati mbalimbali za kihistoria na sababu zao kuchorwa hivyo. Kazi hii itatufaa katika utafiti wetu kwa sababu itatujuvya jinsi mitazamo kuhusu wanawake inakwenda ikibadilika kadri ya wakati.

C. Ndungo, akimnukuu mtaalamu E. Fischer (1959) anadai kuwa mtazamo wa binadamu aghalabu hubadilika katika harakati za kutafuta ukamilifu wake. Katika utafiti wetu tutaduhusa tofauti ya mitazamo baina ya vijana na wazee kuhusu ukombozi wa mwanamke.

E. Katola (2006), alishughulikia swala la udhalimu dhidi ya wahusika wa kike kama unavyojitokeza katika kazi za waandishi wa jinsia zote mbili katika tamthilia za Kiswahili. Aidha, alihakiki mwandishi S. Mohamed katika kazi yake *Kitumbua kimeingia mchanga* lakini hakulenga suala tunalolitafitia linalohusu mitazamo ya vijana na wazee kuhusu ukombozi wa mwanamke. Alijihusisha zaidi na namna mbalimbali ambavyo wahusika wa kike wanavyodhulumiwa. Kazi hii imetufaa kwa kuwa inaongozwa na nadharia ya ufeministi ingawa katika mwelekeo wa kiafrika.

Wataalamu wote hawa hawajajishughulisha na mtazamo wa jamii kuhusu ukombozi wa mwanamke na kwa hivyo kuacha mwanya wa utafiti ambao tunauziba katika utafiti huu.

**1.6 Msingi wa kinadharia**

Uchunguzi wetu umeongozwa na nadharia ya ufeministi. Wamitila (2002), anafafanua ufeministi kama istilahi inayorejelea harakati za ukombozi wa wanawake ambazo zina mwelekeo wa kisiasa. Tuki (1986) wanaeleza ufeministi kama nadharia ya fasihi ambayo inajishughulisha na utetezi wa haki za wanawake dhidi ya ugandamizwaji katika jamii yenye mfumo uliothibitiwa na wanaume.

Wafuasi wa nadharia hiyo wanachukua mwelekeo wa kiharakati na kushambulia baadhi ya asasi zinazochangia katika kumdhalilisha mwanamke. Hakika wanachomaanisha wataalamu hawa ni kuwa, hii ni nadharia inayopendekeza kupiganiwa kwa ukombozi, haki na usawa kati ya wanawake na wanaume.

Nadharia ya kifeministi iliasisiwa kutokana na kuzuka kwa vuguvugu la wafeministi huko Ufaranza na Marekani baada ya vita vikuu vya pili vya dunia. Wafuasi wa nadharia hii kama anavyosema M. Mbatiah (2001), wanachukua mwelekeo wa kiharakati na kushambulia baadhi ya asasi zinazochangia katika kumdhalilisha mwanamke.

Msingi wa nadharia hii unapatikana katika kazi ya Marry Wollstonecraft (1792) anayependekeza kuundwe jamii mpya yenye usawa kati ya wanawake na wanaume. Wollstonecraft ni miongoni mwa waandishi na watetezi sugu wa haki za wanawake. Kazi nyingine za awali ambazo ziliipa nadharia hii nguvu ni pamoja na ile ya Virginia Woolf (1929) na ya Simone De Beauvoire (1947).

Maoni ya Wollstonecraft ni kuwa elimu ni kitu cha msingi katika harakati za ukombozi wa mwanamke na kwamba wasichana wanastahili kupewa elimu sawa na wavulana.

Nadharia ya kifeministi inapinga asasi zozote za jamii zinazochangia dhuluma dhidi ya mwanamke. Wafuasi wa nadharia hii wanahoji kuwa inafaa kuwe na usawa kati ya mwanamke na mwanaume, bila kuzingatia tofauti zao za kimaumbile.

Waasisi na wafuasi wa nadharia hii wanadai kuwa tamaduni nyingi ulimwenguni zinamchukulia mwanamke kama kiumbe duni na wanapendekeza wanawake wajitokeze kupigania uhuru wao dhidi ya wanaume. Tangu nadharia hii iasisiwe, matawi mengi yamechipuka. Kila tawi linapendekeza kinachopasa kuzingatiwa katika uhakiki na pia harakati za kupigania haki na ukombozi wa mwanamke. Kila tawi lina msimamo fulani maalumu na pia wafuasi wake.

Tawi linaloongoza utafiti huu ni lile la kiharakati. Wamitila (2003)anasema kuwa feministi wa kiharakati hutambulishwa na misimamo ifuatayo:-

( i ) Wanawake wananyanyaswa na kukandamizwa na wanaume na kuwa pana umuhimu wa kuielewa nguvu hiyo.

( ii) Mpangilio mzima wa uana wa jinsi watu na vitu vinavyoainishwa umepangwa kwenye misingi ya kiume na kike.

( iii ) Kike ni tokeo la miundo ya kijamii bali sio tofauti kati ya jinsia mbili tofauti.

Anavyomaanisha mtaalamu huyu ni kwamba jinsia imo kwenye kitengo cha maumbile ilhali uana imeibuliwa na jamii ili kuimarisha tofauti ya majukumu kati ya mwanamume na mwanamke.

Tawi hili linakubali ukweli kwamba mwanamke na mwanamume lazima washirikiane katika nyanja mbalimbali maishani. Pana haja ya kubadilisha mtazamo wa jamii ili mwanamke aweze kutambuliwa kama binadamu mwenye haki sawa na mwanamume. Kwa kauli hii basi, hatunabudi katika utafiti wetu kujishughulisha na suala la mitazamo ya vijana na wazee kuhusu ukombozi wa mwanamke. Ufaafu wa nadharia hii ni kwamba itatuongoza kubainisha kuwa wanawake wanadhulumiwa na wanahitaji ukombozi. Vile vile, inaunga mkono ushirikiano wa pamoja katika vita dhidi ya dhuluma kwa wanawake na kwa mujibu wetu., ukombozi unahusisha jamii zima.

## 1.7 Nadharia tete

Utafiti wetu umeongozwa na nadharia tete tatu:

(i) Mtazamo wa vijana na wazee kuhusu suala la ukombozi wa Mwanamke unahitilafiana katika tamthilia hizi tatu.

(ii) Waandishi wa kazi hizi tatu wamewasawiri wahusika vijana Kama msingi wa utetezi wa ukombozi wa mwanamke.

(iii) Watunzi wa tamthilia hizi wametambua kuwa mwanamke Anadhulumiwa na anahitaji ukombozi.

## 1.8 Njia za utafiti

Kwa kiasi kikubwa utafiti wetu umejikita maktabani. Umehusu kusoma na kuhakiki tamthilia tatu zilizoteuliwa kushughulikiwa katika mada yetu ambazo ni; *Migogoro* ya M. Mbatiah (2006), *Kitumbua kimeingia mchanga* ya S. Mohamed (2000) na *Natala* ya K. wa Mberia (1997). Hali kadhalika, tumesoma tamthilia nyingine zinazomulika mada yetu kwa nia ya kuimarisha utafiti wetu.

Pia, tumepitia kazi mbalimbali zilizohakikiwa kwa misingi ya kifeministi zikiwemo tasnifu, majarida, vitabu, makala na kazi nyinginezo zilizoelekea kutunufaisha katika utafiti huu.

Aidha, tumeshirikiana na kuwahoji wataalamu mbalimbali pamoja na waalimu wenye umahiri mkubwa katika nyanja hii. Pia tumekuwa na mijadala na wakufunzi wenzetu bali na kutafuta maarifa katika tovuti.

# SURA YA PILI

## NAMNA MBALIMBALI AMBAVYO WANAWAKE WANADHULUMIWA.

### 2.1.0 Utangulizi

Katika sura hii tunajadili namna mbalimbali ambavyo wanawake wanadhulumiwa katika jamii. Tutazingatia tamthilia tatu zifuatazo; *Kitumbua kimeingia mchanga*, S. Mohamed (2000), *Migogoro*; M. Mbatiah (2006) na *Natala*; K. wa Mberia (1997). Aidha, tutaangazia juhudi zozote wanazofanya au zinazofanywa na wahusika wengine ili kuwanusuru kutokana na hali hiyo. Pamoja na hayo, tutajadili pingamizi zinazozikabili juhudi zao za kujiauni kutokana na hali ya jamii inayowadhulumu.

Nadharia ya ufeministi inasadiki kwamba wanawake wanadhulumiwa kwa namna mbalimbali na mfumo wa jamii unaoongozwa na mawazo ya kiubabe-ume. Dhuluma hizi zinadhihirika katika sura mbalimbali kama tutakavyobainisha katika utafiti huu.

**2.1.1 Kuachishwa shule na kuozwa:** Udhalimu mwingine unaofanyiwa wanawake kama tunavyodokezewa katika *Migogoro* (2006) ni kwamba babake Rukia anajuta kwa kumsomesha binti yake hadi shule ya upili. Anasema angalifanya kama wazee wenzake waliokataa kuwaelimisha mabinti zao labda angalijiepusha na kuchekwa na wenzake. (uk. 25).

Mtaalamu Wollstonecraft (1792) anaamini kuwa elimu ni kitu cha msingi katika harakati za ukombozi wa mwanamke na kwamba wasichana wanastahili kupewa elimu sawa na wavulana. Tunaamini elimu humsaidia mwanamke kuelewa hali yake, haki yake na jinsi ya kujikomboa kutokana na mila kandamizi za jamii yake.

Katika *Kitumbua kimeingia mchanga* (2000), mawazo hayo ya Wollstonecraft hayonekani kutiliwa maanani na wazazi wa Fatuma. Wanawake wanazidi kubaguliwa kielimu. Hali hii inadhihirika katika onyesho la pili ambapo Fatuma na mamake wanaendelea kujishughulisha na maandalizi ya chakula huku Bw. Mambo, Fikirini na Faki wanaendelea kusoma. Yamkini hawawatarajii Fatuma na mamake (Bi. Sikitu) kuwa wakisoma chochote bali na kuwashughulikia jikoni. Hali hii ya kuwatarajia wanawake kuwatayarishia wanaume chakula wakiendelea kujiongezea maarifa labda ndiyo inayowanyima nafasi ya kusoma na kuielewa hali yao na jinsi wanavyodhalilishwa katika dunia inayoendeshwa kwa hatamu za wanaume.
Bw. Mambo anasoma gazeti naye mwanaye na rafikiye wanasoma kitabu cha fasihi.

Kauli ya Bi. Tukaije kwamba hangeweza kuvunja ahadi na wema wa koo zao mbili kwa kumwoza bintiye kwa maskini inatilia nguvu ukweli kuwa katika jamii hii mabinti hawaozwi kwa misingi ya mapenzi bali kwa kuzingatia nguvu za kiuchumi. Hali hii ni ugandamizwaji wa haki za mwanamke kujichagulia mchumba ampendaye.

> Bi. Tukaije: Mtu hutafuta ardhi inayo rutuba kuatika mbegu yake; konde gani yenye rutuba zaidi kushinda yenu? Mtu hukutanisha nguvu hii na nguvu hii ili zizae nguvu zaidi, vipi twende kutafuta udhaifu? Subira ni wenu msiwe na wasiwasi. (uk. 12)

**2.1.2 Kudharauliwa na kutukaniwa ukoo wake:** Katika *Kitumbua kimeingia mchanga* (2000), Bi. Mwatima na Bi. Sikitu wanamdharau Hidaya kwa kudai kuwa yeye ni kiruka njia na hata elimu yake haikumsaidia kwa vyovyote. Isitoshe, wanamtuhumu kuwa ameavya mimba, jambo ambalo hawakulitolea ithibati za kutosha.Tuhuma na shutuma hizi zinatokana na ile dharau waliyo nayo kwa jinsia ya kike hata ingawa wao ni wanawake.

Bi. Mwatima: Basi huyu Hidaya hata kusoma kusimsaidie?

Bi. Sikitu: Kwani kusoma hoja; wakati mwingine hao waliosoma ni afriti zaidi!

Bi. Mwatima: Hashakumu! Watoto watu wazima, nasikia hivi juzijuzi Ameharibu... Hayo mambo ya siku hizi ya kutoa pesa uvyazwe mzigo uliokulemea...(uk. 20)

Hali hii ya kuwadharau na kuwatukana wanawake inaendelezwa katika *Natala* (1997). Mhudumu wa chumba cha kuhifadhia maiti anamtukana Natala kimafumbo. Alijisingizia kuzungumza na wafu humo ufuoni lakini kusudi lake lilikuwa ni kumtusi Natala na jinsia nzima ya wanawake. Kitendo cha kummithilisha mwanamke na maiti ni matusi mabaya.

Bala : [ Anaona maiti yenye kinywa wazi. Anaiendea] Funga kinywa wewe! Unacheka nini? Hujawahi kuona mtu akila andazi. [ Anaona maiti nyingine ambayo imelala kwa namna asiyopenda] Wewe! Usilale kipumbavu kama mwanamke!

Natala: Mwanamke hulala vipi?

Bala: Kama gogo la mgomba. [Anacheka]

Natala: Hayo ni matusi (uk. 19).

Natala anatukanwa na kutukaniwa wazazi wake. Mama Lime anadai kuwa ami na shangaziye Natala wamekataa kimaksudi kuhudhuria mazishi ya Tango licha ya kufahamishwa na Bala kuwa afya ya shangaziye Natala ilikuwa si nzuri. Anazidi kuwahukumu akisema kwamba anasikitika kuwa walioa kutoka kwa ukoo wao. Anadai Natala alirithi ujeuri wake kutoka kwa jamaa zake.

Ile istiari ya kifaranga na mwewe inayotumiwa na Bi. Tukaije akimrejelea mtoto wa kike na namna anavyohusiana na wenzake wa kiume ni dalili ya kuonyesha uduni wa mwanamke. Mshabaha huu unamfanya mwanamke kuonekana dhaifu mbele ya mwanamume; mlinganisho wa mwanamke na mwanamume

unawakilishwa na istiari ya kipanga na paka. Wote hawa wana uwezo mkuu dhidi ya kifaranga.

> Bi. Tukaije: Toka umezaa mayai, hata ukayalalia, hata yakatotoa vifaranga, hata ukavilisha vifaranga na kuvitazama vinakua, na jicho lako juu mbinguni ukivilinda na vipanga na jicho lako chini ardhini ukivilinda na paka...(uk. 9)

Hali hii inamkumba Hidaya wakati Bw. Mambo anapomtaka Bi. Mkubwa amthibitishie ikiwa mbali na kwamba Hidaya ni mtoto wa kimaskini, pia ikiwa ukoo wake nao hauna mashiko mazuri. Mtazamo huo wa Bw. Mambo, unadhihirisha jinsi alivyo na mtazamo hasi kwa wanawake maskini na ile thamani aliyo nayo kwa utajiri na utukufu wa koo. Mtazamo huo una mwelekeo wa kibaguzi na usio wa kiadilifu kwa kuwa hakuna anayechagua anakostahili kuzaliwa.

Kigezo cha kukadiria ubora wa mwanamke wa kuoa kulingana na Bw. Mambo ni utajiri. Anasema;

> "Mchumba tunayemtaka sisi ni mtoto wa watu. Kazaliwa kazalika" (uk. 32).

Hivi ndivyo alivyomwambia mwanawe Fikirini ili kumshawishi avunje uchumba wake na Hidaya, msichana aliyetoka madongoporomoka. Huu ni uonevu kwa wanawake kwa kuwa mapenzi na mali ni mambo tofauti.

**2.1.3 kulimbikiziwa kazi za jikoni na kuhuzishwa na watoto wajeuri:** Wanaume kuwaambia wake zao kuwa watoto wao wanapokuwa wapumbavu ni wa mama zao lakini wakiadilika wanajifaharisha nao. Jambo hili ndilo analoamini Bw. Mambo anapomkejeli mkewe, Bi. Sikitu kwa kumwambia;

Bw. Mambo: Unamsikia ...[Akimwelekea Bi. Sikitu] unamsikia mwanao mpenzi anavyonijibu? Unasikia maneno matamu ya mtoto wako kifunguamimba?

Mawazo kama haya ni dharau kwa mwanamke na yanachimbuko lake katika dini la ukristo, katika Biblia Takatifu kwenye Mithali za Suleimani mlango wa 10:1 "Mwana mwenye hekima humfurahisha babaye; bali mwana mpumbavu ni mzigo wa mamaye". Tunahisi hii si haki kwa mwanamke na kwa hivyo tunayachukulia kama maonevu kwao.

Katika *Kitumbua kimeingia mchanga* (2000) Fatuma, bintiye Mambo, anaagizwa na mamaye Bi. Sikitu kuwaandalia jamaa zake chakula mezani kabla ya wao kurejea kutoka ibada msikitini. Kitendo cha kumshughulisha mtoto wa kike katika kazi za jikoni wakati kaka zake na babake wamo ibadani ni dhihirisho kuwa amenyimwa haki ya kushiriki ibada kama wenzake ili awahudumie jamaa zake.

**2.1.4 Kunyimwa uhuru wa kujichagulia mchumba:** Katika *Kitumbua kimeingia mchanga* (2000), Subira hana hiari kumchagua ampendaye kwa kuwa wazazi wake wamekwisha kufanya mkataba wa ndoa kwa niaba yake. Ingawa Subira mwenyewe hajitokezi wazi wazi kupinga suala hilo lakini tunakisia hakuliridhia.

Hali kama hii ndiyo inayozungumziwa katika tamthilia ya *Migogoro* (2006). Hii ni dhuluma kwa wanawake tukizingatia kuwa mwanamume anayeteuliwa na wazazi wa msichana huenda asimpendeze msichana. Katika tamthilia hii, Rukia anafahamishwa na babake kuwa alishachaguliwa mchumbake na wazazi wake angali mtoto. Mwacharo bin Kiroboto. Alifahamishwa kwamba Mwacharo alikuwa akimsubiri tu amalize mtihani wake ili amchukue. Wazazi wake bila shaka wanaongozwa na mila ambazo waliachiwa na mababu zao na wanaona ni haki yao kuzilinda. Wanatumia kisingizio: "mwacha mila ni mtumwa". Ingawa

mila hii inamdhulumu zaidi mwanamke, pia pana uwezekano kuwa hata wanaume hudhulumiwa.

Tunaamini uhuru wa mwanamke ni uhuru wa mwanamume kwa kuwa wote ni binadamu sawa. Wolgast (1980:18) akimnukuu mwanafilosofia John Locke alidai kuwa;

> " usawa wa binadamu aghalabu uhusishwa na ukweli kuwa wanawake na wanaume ni viumbe wa sampuli na hadhi moja. Kwa hivyo, ikiwa maumbile hayakuwabagua, hakuna haja ya kubaguana." (Tafsiri yetu)

**2.1.5 Kutokubaliwa kujiunga na siasa:** Katika tamthilia ya *Migogoro* (2006), Fatuma anapoelekea mkutanoni wa akina mama ambao unanuia kujadili namna ya kutatua baadhi ya matatizo yao, anakutana na nduguye Mambo ambaye anamwonya dhidi ya kujihusisha na siasa. Anamtahadharisha kuwa siasa ni sawa na mzinga wenye nyuki wakali. Anawafananisha wanaume na nyuki wawezao kumdhuru Fatuma. Matamshi yake yanafichua mawazo yake kuhusu nafasi ya wanawake katika jamii. Hii ni dhuluma kwa akina mama kwa sababu hata kama angekuwa akienda siasani, hiyo ingekuwa ni jukwaa muhimu kwa wanawake kuyaeleza matatizo yao (uk. 13). Maoni yake yanaoana na mila na desturi za jamii nyingi ulimwenguni. Kwa mfano, kulingana na Kabira na Nzioki (1993:5), tamaduni za jamii nyingi za Kenya hazitambui nafasi ya mwanamke katika masuala ya siasa na sheria.

**2.1.6 Kupigwa na kuthibitiwa:** Mambo ni mhusika anayedai kuwa ni halali kwa mwanamume kumchapa mkewe. Hamisi anamweleza Mambo kama mwanamume hodari kwa kumpiga mkewe. Humpiga kila kuchapo mpaka akalazimika kurudi kwao kipigo kinapozidi (uk. 60).

Imani hiyo yake anaipalilia kwa msemo wake: "Ulimwengu wa mwanamke ni jikoni na ulimwengu wa mwanamume ni ulimwengu halisi" (uk. 37). Hii ni imani ya kitaasubi na ni dhuluma kwa wanawake. Katika (uk. 51), Mambo anamwonya Hamisi kuwa akimwacha mkewe kushiriki katika harakati za kuunda chama cha wanawake, atakuja kumtawala nyumbani kwake. Anashadidia kauli hii kwa kuzifananisha nguvu za wanawake na moto. Anasema kuwa wanawake wakiachiwa kupata nguvu wanaume watakuwa taabani. Anashikilia kuwa mababu zao waliwafunza kuwadhibiti wanawake wakae nyumbani waokote kuni, wateke maji, wapike, watunze watoto, wafue, walime, waangalie waume zao na wala wasitoke kwenda nyanjani kuunda vyama.

Mambo anayasema haya yote kwa kusingizia kuwa anaheshimu mila na desturi za mababu ambazo zinamtaka mume awe kiongozi na mke awe mfuasi. Kauli hii pia inatiwa nguvu na mawazo ya Biblia (Waefeso 5:22) na (Wakorintho wa 1, 14:34).

Katika *Natala* (2000), Wakene, nduguye Tango, anamtongoza shemejiye Natala. Huu ni ukosefu wa heshima kwa mke wa nduguye na pia kwa nduguye Tango ambaye alikuwa mjini akitafuta riziki. Dharau kama hii ndiyo anayozungumzia A. Mazrui (1982) katika *Kilio cha Haki.* Lanina anadhihakiwa na kudharauliwa na wanaume wateja kwenye kioski cha mzee Ingeli. Wanaume hao wanamuuliza Lanina sababu ya kujitoa kwenye orodha ya menyu kana kwamba yeye alikuwa miongoni mwa bidhaa zilizouzwa.

**2.1.7 Kudhulumiwa kimapenzi na kinyimwa uhuru:** Mhudumu wa chumba cha kuhifadhia maiti alianza kwa kumkejeli Natala kwa maswali yanayomkera. Maswali hayo yalinuiwa kumuudhi na kumuumbua kama binadamu mwenye haki ya kuhudumiwa inavyostahili. Anamlimbikizia shutuma za uongo kuwa anamtukana na kwamba anamdharau mhudumu huyo pamoja na kazi yake, jambo ambalo hakulifanya kamwe na baadaye alidai pesa kama hongo. Aidha, alimtaka

Natala kumhonga kimapenzi ili amtwalie maiti ya mumewe. Natala anajipigania na kukwepa juhudi zake za kumpapasia ndani ya ofisi yake. Ushujaa wa Natala unaweza kumithilishwa na ule wa Lanina katika *Kilio cha Haki* (1997) alipopigana na askari aliyetaka kumnajisi alipowekwa korokoroni kwa madai ya kuchochea maasi ya wafanyikazi katika shamba la Delamon.

Katika *Kitumbua kimeingia mchanga* (2000), Bi. Mwatima anamshtumu na kumlaani Hidaya kwa kumwona akiandamana na vijana wa kiume njiani. Anamsingizia kuwa amekwisha kuharibika na kumshuku kuwa 'kitumbua' chake kimekwisha kuingia mchanga; yaani amekwisha uharibu ubikira wake. Hali hii ndiyo aliyokuwa akiizungumzia A. Mazrui (1982) katika tamthilia ya *Kilio cha Haki* alipomsawiri mhusika Lanina ambaye utangamano wake na wafanyikazi wenzake pamoja na wanaharakati wa kutetea haki za wafanyikazi ulipomzushia shutuma kutoka kwa wazazi na mumewe. Lanina analaumiwa na wazazi wake pamoja na mumewe Mwengo kuwa amegeuka malaya. Kitendo cha kumnyima mwanamke uhuru wa kutangamana na wenzake wa kiume ni dhuluma.

**2.1.8 Mila zinazohimiza kurithi wajane:** Binadamu si bidhaa na kwa hivyo tabia ya wanaume kurithi wanawake ni kuwashushia hadhi yao kama binadamu. Hali hii inawabagua wanawake tukizingatia kuwa wanaume hawarithiwi. Hapa tunarejelea mhudumu wa ufuoni ambaye anajivunia kumrithi mke wa marehemu nduguye ambaye inaelekea alikufa kwa ugonjwa mbaya. Tabia kama hii inahatarisha afya ya mume na mke na kwa hivyo inafaa kukomeshwa. Huu ni utamaduni ambao hauna nafasi katika enzi hii na ni sawa na kuwanyima wanawake uhuru wao kujiamulia wapendavyo.

Ukoo wa familia ya 'marehemu' Tango Mwina ukiongozwa na Mama Lime unamtaka Natala akubali kuolewa kama mke wa pili na ndugu ya mumewe; yaani Wakene. Baada ya Natala kukatalia mbali ombi lao, wanashirikiana kumfurusha

kutoka nyumba yake pamoja na kumnyang'anya hati-miliki ya shamba la mumewe.

Mila na desturi za kiafrika zinamdhalilisha mwanamke kwa kumpa nafasi ya jikoni tu. Kama anavyosema Mama Lime (uk. 39). kwamba, furaha ya mwanamke ni kuwa na makazi, kula na kushiba, kuvaa nguo na kupata watoto. Maoni kama haya yanamfunga mwanamke na kazi ya nyumbani huku mchango wake kama mfanyi kazi, mwanasiasa na kiongozi ukipuuzwa. Hali kama hii tunaihesabu kama dhuluma kwa mwanamke.

**2.1.9 Umaskini:** Katika *Migogoro* (2006), Fatuma anaeleza shida za akina mama ambazo anasema zinatokana na kushindwa kupata mahitaji ya lazima (uk. 14-15).

> Fatuma: Nani hajui kwamba umasikini umejenga zizi katika maisha ya wanawake?
>
> Mambo: Hakuna asiyejua.

Umasikini anaozungumzia Fatuma sio wa majaaliwa bali unasababishwa na mfumo wa ugawaji mali uliobuniwa na jamii inayoongozwa na wanaume waliotawaliwa na taasubi.

Jamii nyingi ulimwenguni zinapendelea urithi kuwaendea wanaume na hivyo kuwapelekea wanawake kote ulimwenguni kuishi maisha ya ulitima. Sio tu katika suala la mirathi ambapo wanawake hubaguliwa lakini hata katika umilikaji wa raslimali muhimu za uzalishaji mali kama vile ardhi. Kama wanavyosema W. Kabira na E. Nzioki (1993:19);

> " .... Sisi tunajishughlisha na juhudi za pamoja za kupinga tamaduni na mila zinazohusu urithi wa mali na juhudi za wanawake kubadilisha utamaduni huo dhalimu" (Tafsiri yetu).

Katika tamthilia ya *Natala* (1997), Natala ananyimwa haki ya kumiliki nyumba ya mumewe. Tila anadai kuwa Natala hana haki ya kumfukuza kutoka katika nyumba ya ndugu ya mumewe; yaani Tango. Hii ni dhuluma anayofanyiwa Natala hasa tukizingatia kuwa yeye yuko kwake. Jambo la kustaajabisha ni kwamba, dhuluma hii haifanywi na mwanamume bali inatoka kwa mwanamke mwenzake. Jambo hili lina maana kwamba wanawake hudhulumiana wao kwa wao (uk. 5)

**2.2.0 JUHUDI ZINAZOFANYWA KUMKOMBOA MWANAMKE:** Mbali na kwamba wanawake wanakandamizwa kwa njia mbalimbali kama tulivyodhihirisha katika tamthilia hizi tatu, tunatambua juhudi zinazofanywa na wanawake na wahusika wengine kuwakomboa. Waandishi hawa katika tamthilia zao hawajafumbia jicho juhudi zinazofanywa na baadhi ya wahusika wake ili kuwanusuru wanawake kutokana na dhuluma zinazowakabili.

**2.2.1 Wanawake kushirikiana na wanaume:** Kupitia kwa mhusika Fatuma, mwandishi anatufahamisha kwamba wakati wa wanawake kuanza kutafuta uvumbuzi wa matatizo yao umewadia. Anapendekeza akina mama kujumuika pamoja na kushirikiana na watu wengine wenye nia njema ili kutatua matatizo yanayowakabili. (uk.13).

Fatuma anamwakikishia nduguye Mambo kwamba awamu ya kutenda imewadia na hiyo ndio sababu wanawake wanakutana kila wanapokuwa shughulini zao za kila siku na kujadili matatizo yao. Anasema kuwa wao, kinyume na wanaume ambao huchelea kujadili shida zao hadharani kwa kuhofia kufichua udhaifu wao, wanawake huzijadili wanapokutania kisimani, sokoni na hata wanapokutania njiani. Hii ni dhihirisho tosha kwamba wanawake wametambua shida zao na wamekwisha kuchukua hatua ya kwanza.

Ili kutatua tatizo lao, Fatuma (uk. 16) amejitwika jukumu kwa niaba ya wanawake wote wa Makato kuzungumza na viongozi wa makanisa na wanawake kutoka sehemu nyingine za nchi zilizoendelea. Ametambua kwamba tatizo la wanawake linafungamana na tofauti za kimaendeleo kutoka sehemu moja hadi nyingine. Anavyomaanisha hapa ni kuwa ukosefu wa maendeleo kwenye sehemu wanakoishi wanawake kunawasababishia umaskini ambao ni kikwazo kwa ukombozi wao.

Pamoja na viongozi wa makanisa, madiwani na wabunge wanafaa kuhusishwa katika juhudi za kutafuta suluhu juu ya matatizo ya wanawake. Kama anavyopendekeza Fatuma ni kwamba, wanawake wa Makato wanafaa kubuni kikundi chao ambacho kitawaleta pamoja ili kubadilishana mawazo. Chini ya kikundi chao wangechanga pesa za kuanzisha miradi ya kuwapunguzia umaskini.

Katika tamthilia ya *Migogoro* (2006), wapo wahusika wengine waliojaribu kumtetea Natala dhidi ya dhuluma zilizomkabili. Ba. Mkwe (Mzee Balu) alimtetea Natala dhidi ya shutuma alizotolewa na Jamaa za mumewe baada ya kukataa shauri lao la kufungua Jeneza ili kutazama mwili kabla ya mazishi. Mzee Balu hakujali kukabiliwa na lawama baada ya kudai kwamba ilikuwa muhimu kuheshimu hisia za mke wa 'marehemu'.

Gane na Bala walimsaidia Natala asinyang'anywe cheti cha kumiliki shamba la mumewe. Bala anampongeza Natala kwa kulinda vilivyo heshima yake na ya wanawake kwa jumla (uk. 23) wahusika hawa wote wanadhihirisha juhudi zao za kuunga mkono ukombozi wa wanawake.

Matangazo ya vyombo vya habari kuhusu vyama vya ushirika vya wanawake ni muhimu. Shirika la utangazaji la B.B.C lilitangaza habari za chama cha Ngao na kukifanya kijulikane kote mpaka shirika la *Helpline* likatuma msaada wake.

Katika *Migogoro* (2006), Natala alisimama kidete kupigana na mwanamume aliyetaka kumdhulumu. Mhudumu wa chumba cha kuhifadhi maiti alitaka kuhongwa kwa kupewa pesa ili aiachilie maiti ya mumewe Natala lakini hakufaulu. Vivyo hivyo, tamaa yake ya kumnyanyasa Natala kimapenzi kabla ya kumhudumia ilikabiliwa kwa upinzani mkali. Natala alipigana kwa jino na ukucha kuhifadhi heshima yake na ya wanawake kwa jumla (uk. 23).

Juhudi zingine za mwanamke kujikomboa zinadhihirika wakati Natala anapokabiliwa na Mama Lime kwa shauri la kuolewa mke wa pili na shemeji yake. Natala anachukua msimamo thabiti wa kuyakatalia mbali matakwa yake na ya ukoo mzima. Ingawa walimtisha kwa kumfurusha kutoka nyumba na ardhi ya mumewe, hakulegeza msimamo wake kuwa ana haki ya kuyaendesha maisha yake pasipo kuhitajika kujinyenyekeza na kukubali kutii mila zinazomdhalilisha yeye na wanawake kwa jumla.

**2.2.2 Kujiendeleza kimasomo na kutotia matumaini katika ndoa:** Wanawake kuendelea na masomo ya Chuo Kikuu na kusomea taaluma zitakazowapa kazi zenye kipato kizuri. Hii ni mojawapo ya mikakati anayonuia kuitumia Farida ili kujiondolea umaskini ambao umekwisha kutambuliwa kama kikwazo cha ukombozi wa mwanamke. Farida anataka kujiunga na chuo kinachotoa mafunzo ya Benki huko mjini Nairobi kama msingi wa kupata kazi nzuri kama ya Mwaliwa ambaye ni karani wa Benki ya ushirika.

Katika tamthilia ya *Migogoro* (2006), mwandishi anawashauri wanawake kutokimbilia ndoa za mapema kabla ya kupata elimu ya maana. Kama anavyosema Farida katika (uk. 19). itambidi kwanza asubiri awe mtu kamili kabla ya kufikiria kuolewa.

Farida: "....niwe mtu kamili kuolewa katika mpango huu kumetiwa kwenye mabano wanielewa?

Rukia: Nisikuelewe kwani ni fizikia unafunza? Kuolewa kukifungiwa kwenye mabano kunaweza kuwepo au kusiwepo (uk 19).

**2.2.3 Kufuata mifano ya wanawake waliojikomboa:** Ukombozi wa mwanamke utatokana na wao kuiga mifano ya wenzao waliofanikiwa. Katika tamthilia ya *Migogoro* (2006), Dadake Farida anafanya kazi nzuri na shirika la posta. Malipo yake ni mazuri yalimwezesha kujinunulia kiwanja cha gharama kubwa mjini. Isitoshe, Farida anasisitiza kuwa dadake amenenepa sio kimwili tu bali pia kiuchumi. Farida na Rukia wanaazimia kusoma kufa na kupona kama njia ya kujipatia taaluma ya maana na uhuru kamili (uk. 21).

**2.2.4 Kuanzisha miradi ya kujisaidia:** Hamisi katika mazungumzo yake na mkewe Fatuma (uk. 74) anapendekeza chama chao cha Ngao kijitwike jukumu la kushughulikia tatizo la uavyaji mimba miongoni mwa wasichana. Mwelekeo kama huu wa ushirika wa wanawake wenye azima ya kumkomboa mwanamke unaungwa mkono na baadhi ya wanaume wenye mawazo ya kifeministi kama anavyodhihirisha Hamisi.

Ushauri unaotolewa na Hamisi kwa mkewe ni mfano wa juhudi za kumkomboa mwanamke. Tumekwisha kutambua kuwa mojawapo ya vikwazo vinavyowalemaza wanawake ni umaskini. Ikiwa watafanikiwa kupigana na umaskini huo, hiyo itakuwa ni hatua ya kimsingi kuelekea ukombozi wao.

Wanawake ambao hawakusoma utotoni wao wanatakiwa wachukue nafasi ya kujisomesha hata wakiwa watu wazima. Hamisi anamshauri nduguye Amina afundishwe kusoma na kuandika na bintiye Rukia punde tu amalizapo mtihani. Amina anafurahia ushauri huo na kuanza masomo yake. Hatua hii ni mojawapo ya

juhudi muhimu zinazowapelekea wanawake kujikomboa kimawazo na kuepukana na umaskini unaowarudisha nyumba kimaendeleo (uk. 57). E. Gachukia (1993:56) anasema kwamba elimu kwa mwanamke humfungulia milango ya ufanisi katika kiwango cha kibinafsi na kuinua uchumi wa nchi. Anaeleza kuwa elimu ni ufunguo wa nafasi nyingi za kujiendeleza kimaisha kupitia ajira nzuri.

**2.2.5 Serikali kutoa ufadhili kwa wanafunzi bora:** Hatua ya serikali kutoa ufadhili wa masomo kwa Rukia binti Hamisi ni dhihirisho la juhudi zake katika ukombozi wa mwanamke. Pengine wasichana wafanyao vyema mitihani huwa hawaendelei na masomo ya juu kwa sababu ya ukosefu wa karo. Rukia anadai kuwa wazazi wake hawakuwa radhi kumruhusu kusomea taaluma itakayompa kazi ya kipato kizuri. Bali na kuwa wazazi wake wanashindwa kugharamia masomo yake ya juu, anaeleza kuwa mapenzi yao ni kwamba asomee taaluma ya ualimu wa shule ya msingi. Hata hivyo hatua hii ya serikali lazima iandamane na idhini ya wazazi kuwaruhusu watoto wao wa kike kwenda nje ya nchi kusomea elimu ya Chuo Kikuu inapobidi. Kama anavyoeleza mwandishi ni kuwa wazazi wa Rukia hawanabudi ila kumruhusu binti yao kwenda masomoni.

Tunaichukua nia yao kama hatua ya kimapinduzi dhidi ya tamaduni zinazomkataza mwanamke kupata elimu ya juu na kupewa uhuru wa kuchagua kima cha elimu anayotamani.Ufadhili kutoka mashirika ya nchi zilizoendelea ni mfano wa juhudi za nchi hizo kushiriki katika ukombozi wa mwanamke. Shirika la kimarekani la *Helpline* lilimtuma Bw. Alex Taylor kuleta ufadhili wao kwa chama cha Ngao. Ufadhili wao wa shilingi laki moja unusu ni dalili ya utambuzi wa taifa hilo kwa ukombozi wa mwanamke.

Chama cha Ngao kinaazimia kukopa pesa benki ili kupanulia miradi yake pindi kitakapojenga nguzo imara. Azimio hili jema la chama cha Ngao limevutia mkopo

kutoka kwa Hamisi wa shilingi elfu mbili. Jambo hili linanuia kuboresha maisha na hali ya wanawake kama msingi wa ukombozi wao. (uk. 77).

**2.2.6 Kupuuzilia mbali tamaduni kandamizi:** Katika tamthilia ya *Kitumbua kimeingia mchanga* (2000), Bi. Sikitu anaelekea kuelewa jinsi mwanamke alivyokandamizwa na utamaduni unaomtaka mwanamke kuwa bikira kabla ya ndoa na hiyo ndiyo sababu anamuuliza mumewe (Bw. Mambo) swali hili ambalo ni dhihirisho kamili kuwa Bi. Sikitu anapinga uonevu dhidi ya mwanamke.

> "*Na kama kutia kitumbua mchanga, kwa nini hawi Fikirini mwanetu ndiye mtia-mchanga? (uk. 46).*

Hidaya ni mhusika mwingine anayepinga maonevu wanayofanyiwa wanawake kwa kulalamikia shutuma za Bi. Haja na mpenziye Fikirini. Hidaya anamlaumu mchumbaye kwa kumuuliza ikiwa Kitumbua chake kimeingia mchanga. Swali hilo alilichukulia kama matusi kwa wanawake (uk.54) anamkashifu Bi. Haja kwa kueneza uvumi kwamba alimwona amezungukwa na wanaume na kumdhania kuwa amekitia 'kitumbua' chake mchanga.

Baba Hidaya amekwisha kutambua kuwa wanawake wananyanyaswa na mila na tamaduni za kale. Akimjibu Bw. Mambo aliyeingiwa na kiwewe baada ya harusi ya Baddi na Zubeda kuwa kinyume na matarajio yake. Anataja tabia ya wazee ya ung'ang'anizi wa ukale na kuweka hadharani siri za watoto wao wa kike kama upumbavu unaoendelea kuwatia wazee aibu. Anaonelea ya kwamba wazee wanastahili wajutishwe na aibu inayowafika kama ilivyompata Bw. Mambo. Maoni yake ni kwamba kanuni hizi zinazomsonga mwanamke hazina maana na zafaa kutupiliwa mbali. Kwa kauli hii Baba-Hidaya anajidhihirisha kama mtetezi wa wanawake.

Baba - Hidaya: Haya ni makosa yetu sisi wazee! Kwa nini tunaendeleza kitiba hichi cha kusisasambura siri za watoto wetu na kujipaka kinyesi sisi wenyewe?

Bi. Haja: Sheria ya enzi!

Baba-Hidaya : Wacha basi itupige sisi wenyewe... Tunalia na nani basi? (uk. 63).

**2.3.0 CHANGAMOTO ZINAZOZIKABILI JUHUDI ZA KUMKOMBOA MWANAMKE:** Juhudi za kumwokoa mwanamke kutokana na dhuluma tulizozijadili hapo juu hazijakuwa rahisi.Hapa tutafafanua baadhi ya changamoto zinazozikabili juhudi hizo.Tunaamini kuwa vikwazo hivyo vitakapoondolewa, ukombozi wa wanawake utakuwa hauna budi kupatikana.

**2.3.1 Uhafidhina wa wazee:** Katika tamthilia ya *Kitumbua kimeinga mchanga*(2000), utawala wa mabavu wa wazee wahafidhina unamithilishwa na hatari ya bahari inayodhibiti, kuangamiza na kuua ipendavyo. Pia, bahari inashabihishwa na Jitu nene; yaani jibaba lisilo ukomo wa kuamrisha wanawake kufuata matakwa yake. Bahari na Jitu ni jazanda zinazowakilisha nguvu za wazee zinazopinga juhudi za ukombozi wa mwanamke katika jamii.

Fikirini: Aaaa, basi tu nafikiri hivyo- mimi naona bahari ni kama kiumbe; mithili ya jitu kubwa lenye ukubwa usio mwanzo wala mwisho. Kama vile jibaba lisilo ukomo wa amri na utawala wa mabavu (uk.36).

Bw. Nia anathibitisha chanzo cha pingamizi hizi anaposema kwamba tatizo kuu linatokana na wazee ambao kwa maoni yake wamegubikwa na pazia la wakati uliopita, amali zake, mila na desturi zake. Anaongeza kwamba, hata ingawa vijana wanajizatiti kumulika mwangaza, mwangaza huo ni dhaifu kwa wazee wao

kuuona. Maoni haya yanatuelekeza kufikiri kuwa juhudi za kujikomboa kwa wanawake zinakabiliwa na fikira za wazee za kihafidhina (uk. 45).

Tamthilia ya *Migogoro* (2006) inaanganzia pingamizi hizo kupitia kwa mhusika Mambo. Mambo ni mtetezi wa ukale na kwa hivyo angali anashikilia kuwa mbali na mabadiliko yaliyopo kuhusu nafasi ya mwanamke katika jamii, anaonelea kuwa wanawake wakiachiliwa waungane, watapata nguvu na kuwa tisho kwa wanaume. Mambo anadai kwamba mababu zao waliwafunza kuwadhibiti wanawake ili nafasi yao ibakie kuwa nyumbani. Kazi yao kuu iwe ni kuokota kuni, kuteka maji, kupika kutunza watoto, kufua, kulima na kuangalia waume zao na wala sio kwenda nyanjani kuunda vyama. Tunahisi kwamba maoni haya yake yamepitwa na wakati kwa kuwa hatuwezi kuendelea kushikilia thamani za kale zisizo na faida na ambazo zinamdharau mwanamke kama binadamu asiyekamilika. Jambo hili ni kinyume cha imani ya wafeministi wa kiharakati ambao hushikilia mawazo kwamba; kike ni tokeo la miundo ya kijamii bali sio tofauti kati ya jinsia mbili tofauti.

**2.3.2 Kuvunjwa moyo na wanaume:** Wanawake wanaotaka kushiriki siasani kama njia ya kuyaeleza matatizo yao wanavunjwa moyo na wanaume wanaowakanya dhidi ya kujiunga na siasa. Mambo anamhofisha mapema Fatuma kuwa kushiriki siasa ni sawa na kuingia mzingani wenye nyuki wakali. Anawafananisha wanaume na nyuki wawezao kuwadhuru wanawake. Nia ya Mambo ni kumwonyesha mwanamke hana nafasi katika siasa. Jambo hili ni pingamizi katika ukombozi wa mwanamke.Mambo anaonya kuwa iwapo kikundi cha kina mama kitaonyesha kuunga mkono wanasiasa au kuwapuuza wengine kitakabiliwa na uadui kutoka kwa wanasiasa hao.

**2.3.3 Ukosefu wa elimu kwa viongozi wa wanawake:** Baadhi ya viongozi wa vyama vya wanawake hawana elimu ya kutosha. Fatuma anakiri mbele ya nduguye Mambo kuwa mchango wake kisiasa ni mdogo kutokana na elimu yake ya darasa la saba ikilinganishwa na wanasiasa wenye shahada zao na mapesa. Hali hii ya wanawake kujihisi wamepungukiwa na uwezo kwa ajili ya ukosefu wa pesa na elimu ni kikwazo kikubwa dhidi ya ukombozi wa wanawake (uk. 17).

Mila na tamaduni zinazowataka wazazi kuwachagulia binti zao wachumba ni kikwazo kikubwa juu ya uhuru wa mwanamke. Katika tamthilia ya *Migogoro* (2006), Rukia alifahamishwa na babake kuwa anasubiriwa na Mwacharo bin Kiroboto amalize masomo ili wafunge ndoa. Anamwonya vikali dhidi ya uhusiano wake na kijana Mzula ambaye ni kufu yake. Hatua hii ya wazazi ni changamoto kwa ukombozi wa mwanamke. (uk. 24).

Upinzani mwingine unahusishwa na baadhi ya vijana wa kiume ambao bado wana imani na mila za kale na wanahofu kuzivunja. Wamezibwia baadhi ya amali na tamaduni za jamii zinazomtweza mwanamke na wao hugeuka kuwa kikwazo kwa ukombozi wa mwanamke.Fikirini ni mmoja wa vijana walioathiriwa na mawazo ya jamii yake kuhusu 'usafi' wa kitumbua kabla ya ndoa. Hili ni jambo analolikubali katika dondoo hili:-

> Hidaya: Makosa ya nani?
> Fikirini: Makosa ya jamii kwa jumla... makosa ya kila mtu kwa hakika... wadogo kwa wakubwa, wake kwa waume.

Fikirini anaelekea kukiri kuwa changamoto zinazozikabili juhudi za kumkomboa mwanamke zinatokana na mfumo mzima wa jamii kuhusu nafasi ya wanawake. Anashadidia pia kuwa jamii imeweka kanuni kali ambazo kila mtu anaogopa kuzikiuka kwa kuhofia jicho kali la jamii nzima. Fikirini anailaumu jamii nzima kama udhuru kwa kumdharau mchumbake Hidaya. Kwa kusema hivyo ana

halalisha kitendo chake cha kumdharau mwenzake. Anakubali kuwa vijana wanaunga mkono dhuluma kwa wanawake huku wakifahamu ni makosa kufanya hivyo.

Kwa mujibu wa tamthilia ya *Natala* (1997) dini ni kikwazo kikuu cha usawa baina ya wanaume na wanawake. Kama anavyoeleza mhusika Bala (uk. 19) ni kuwa, dini inafundisha kuwa mwanamke alitokana na kifupa cha mwanamume. Biblia, (Mwanzo: 2:21) mawazo haya yanatumiwa na wanaume kuwanyanyasa wanawake na hivyo kuifanya dini kuonekana kama kikwazo kwa usawa baina ya mwanamke na mwanaume.

**2.3.4 Kutopewa uhuru wa kuchagua maisha yao:** Rukia anaeleza vita vyake na wazazi wake kumkataza kufikia lengo lake la kuufukuza umaskini kwa kusoma kwa bidii na kusomea taaluma ya uuguzi iliyo na kipato kizuri. Wazazi wake wanampinga kwa sababu yeye ni mtoto wa pekee na wasingetaka aende mbali nao na isitoshe walikuwa wamemchagulia taaluma ya ualimu ambayo kulingana na maoni ya Rukia haina malipo mazuri (uk. 22).

**2.3.5 Ukosefu wa mtaji:** Ingawa ushirika wa wanawake ndio nguvu yao, hawawezi kuendesha mradi wowote wa kuzalisha fedha mpaka wawe na pesa za kuanzisha shughuli hiyo. Hali kama hii ndiyo iliyokikumba chama cha Ngao hadi kikaanza kutegemea mikopo na ufadhili kutoka kwa wahisani. Kama tulivyokwisha kueleza awali mojawapo wa udhaifu unaowapelekea wanawake kunyanyaswa na wanaume ni kuwa wategemezi. Kwa hivyo, ili kujikwamua kutokana na hali hiyo wanahitaji kujikomboa kiuchumi.

### 2.3.7 Hitimisho

Katika sura hii tumejadili njia mbalimbali ambazo wanawake wamekandamizwa katika jamii kwa mujibu wa tamthilia tatu zilizoteuliwa. Ingawa kila mwandishi ameangazia dhuluma kwa wanawake kwa mkabala tofauti na wenzake, kuna mambo fulani ambayo wanaelekea kukubaliana. Aidha, kina ambacho wameshughulikia mada hiyo kinatofautiana.

Katika tamthilia ya *Kitumbua kimeingia mchanga* (2000), S. Mohamed amezungumzia dhuluma kadhaa zinazomkabili mwanamke. Baadhi ya dhuluma hizo ni kudunishwa na wanaume wenye taasubi, mila na tamaduni zinazowataka wanawake kuchaguliwa wachumba, kuozwa kwa matajiri na kuthamini ubikira wa mwanamke kabla ya ndoa miongoni mwa nyingine.

Katika tamthilia ya *Migogoro* (2006), mwandishi anataja dhuluma kadhaa kama vile wanawake kuteswa na waume zao, kubaguliwa, kuishi kama kwamba wao sio binadamu kamili; yaani kudhalilishwa na kuishi katika umasikini uliokithiri.

Tamthilia ya *Natala* (1997) inazungumzia dhuluma zinazofanywa na baadhi ya wanaume wenye taasubi, kunyanyaswa kimapenzi na mila zinazowabagua wanawake kuhusu urithi wa wajane na mali.

Pamoja na dhuluma hizi, waandishi hawa wanatambua juhudi zinazofanywa ili kubadilisha hali ya wanawake katika jamii. Baadhi ya hatua zinazopendekezwa ni pamoja na kuwapa wanawake elimu, kuwashirikisha kwenye miradi ya kuwainua kiuchumi, kuunda vyama vya ushirika vinavyoshughulikia matatizo yao na kuvutia ufadhili kutoka kwa wahisani. Mikakati mingine ni pamoja na kupinga mila na desturi zinazowanyanyasa wanawake. Vile vile, kuwahimiza wanawake kusimama kidete kupigania uhuru na haki zao kwa kukataa kunyanyaswa na wanaume.

Juhudi hizi zinakabiliwa na changamoto kadha wa kadha kama vile; imani ya dini kuhusu usawa wa mwanaume na mwanamke, kutojua kusoma miongoni mwa viongozi wa vikundi vya wanawake na ukosefu wa mtaji wa kuanzisha miradi ya kujiinua kiuchumi. Bali na pingamizi hizi kuna swala la utamaduni na mila kandamizi pamoja na taasubi ya kiume miongoni mwa jamii. Vile vile, tumetambua wahusika wa kike kuhusika kuwanyanyasa wanawake wenzao na hivyo kuwa pingamizi kwa ukombozi wao.

Haya ndiyo maswala ambayo nadharia ya ufeministi inahusika nayo. Nadharia hii kama tulivyotangulia kusema katika msingi wake inashikilia kuwa wanawake wanadhulumiwa na wanahitaji kujikomboa. Ule ukombozi nao unahitaji ushirika ili kuufanikisha. Jambo hili ndilo analozungumzia M. Mbatiah (2006) katika tamthilia ya *Migogoro* anapoeleza azimio la wanawake kuunda chama kitakachoshughulikia masaibu yao.

# SURA YA TATU

## MITAZAMO YA VIJANA KUHUSU UKOMBOZI WA MWANAMKE

### 3.1.0 Utangulizi

Katika sehemu hii tutaangazia mitazamo ya vijana kuhusu ukombozi wa mwanamke. Aidha, tutajadili tofauti baina ya mitazamo ya vijana wa kike na wa kiume. Vile vile, tutadadisi sababu za kutofautiana au kufanana kwa mitazamo baina yao.

**3.1.1 Kusoma na kupata kazi nzuri:** Katika tamthilia ya *Migogoro* (2006). Mtazamo wa Farida na Rukia kuhusu ukombozi wa mwanamke unaweza kuelezwa kwa kuzingatia ndoto zao maishani (uk. 19-21), vijana hawa wameamua kukabiliana vilivyo na juhudi za wazazi wao za kuwarejesha nyuma katika maisha ya kale.

Vijana hawa wametambua umuhimu wa elimu ya juu kama silaha mwafaka katika vita dhidi ya ugandamizwaji wa haki zao. Baada ya kuhitimu kidato cha nne na kupata matokeo mazuri wangejiunga na vyuo vikuu ili kusomea taaluma zitakazowapatia mishahara mizuri. Wanaamini umaskini, ushamba na ukosefu wa elimu ndio sababu kuu zinazochelewesha ukombozi wa mwanamke. Mwelekeo huu unaafikiana na mawazo ya mtaalamu E. Flexner (1982:ix) ambaye anadai kuwa:

> Ni kazi bora tu ambayo ina uwezo wa kumwezesha
> mwanamke mwenye elimu kujiepusha na kero nyingi
> zinazohusishwa na maisha ya vijijini yanayomdhalilisha.
>
> (Tafsiri yetu)

**3.1.2 Kufa au kubadilika kwa mila zinazomgandamiza mwanamke.** Kuhusu mila na desturi zinazomnyima mwanamke haki ya kupata elimu, vijana wa kike wakiwakilishwa na Rukia katika tamthilia ya *Migogoro*, wanaamini mila za kale zafaa zife. Kama anavyodai Rukia ni kwamba sayansi inafundisha kuwa mabadiliko ni jambo la kawaida ulimwenguni na kwamba vitu visivyokubali kubadilika aghalabu hufa. Vivyo hivyo mila na desturi za jana zinafaa zife kwa utundu wake wa kukataa kuzipisha mila za leo. Mila za leo kulingana na vijana hawa zinamruhusu mwanamke kujichagulia kuingia au kutoingia katika ndoa kuchagua mchumba na kuendelea na elimu kadiri ya uwezo wake.

**3.1.3 Kupinga kuchaguliwa wachumba na kuozwa mapema.** Nia ya vijana ni kupinga juhudi za wazazi wao kuwachagulia wachumba na kuwaoza mapema. Badala yake wangependa waachiwe uhuru wa kujichagulia wapenzi na kusoma hadi watakaporidhika. Katika tamthilia ya *Migogoro* (2000), Farida anadhihirisha uchungu wake katika msururu wa maswali ya balagha aliyoyauliza katika mazungumzo yake na shogaye Rukia;

> FARIDA: "... Wanaishi jana hawataki kupambazuke.
> Badala ya kuyakaribisha machweo kwa
> furaha, wanayalaani. Kazi bure.
> Sayari Dunia utaifunga kwa minyororo
> gani iache kulizunguka jua? Breki gani
> utakanyaga kupunguza mwendo wa wakati?
> Wazee: Mtakubali lini kwamba jana ni jana
> na leo ni leo? Mtakubali lini kwamba
> chakula cha kimwili na cha kiroho
> mlicholishwa sicho kifaacho kwa watoto
> wenu?..." (uk 22).

Ingawa kulingana na mtazamo wa vijana pana haja ya kubadilika na wakati, pia, isieleweke kama kwamba mila na desturi za kale zote ni mbovu. Kama

anavyopendekeza mhusika Hidaya katika tamthilia ya *Kitumbua kimeingia mchanga* (2000) anasema kwamba hata ingawa tatizo la ukandamizwaji wa wanawake linatokana na utamaduni uliorithiwa kutoka kwa mababu, haina maana kutupilia utamaduni wa kiafrika mbali kama kwamba ni mbaya lakini kinachofaa ni kuchagua mazuri ya zamani na kuyaendeleza pamoja na mazuri ya sasa.
(uk. 52).

Mawazo haya yanaafikiana na yale ya mtaalamu S. Mamuya (1974:22.).Kuhusu uchaguzi wa mchumba, anasema kwamba zamani ilikuwa ni desturi ya kijana kuchaguliwa mchumba na wazazi wake lakini siku hizi wana uhuru wa kuchagua wachumba. Anaendelea kusema kuwa swala hili aghalabu huleta mgogoro baina ya wazazi na vijana lakini ingawa uamuzi wa mwisho unamtegemea kijana, ni jambo la busara kushirikisha wazazi katika shughuli hiyo.

**3.1.4 Kukuza uhusiano mwema baina ya wanawake na wanaume.** Tamthilia ya *Kitumbua kimeingia mchanga* (2000) inafafanua maoni ya vijana kuhusu namna ambavyo wanawake na wanaume wanavyopasa kuhusiana. Kupitia mhusika Hidaya, Vijana wanaupuuzilia mbali ule mlinganisho wa uhusiano wa mwanamume na mwanamke. Mawazo ya wazee kuwa uhusiano baina ya mwanamume na mwanamke ni sawa na wa paka na samaki au kiberiti na petroli ni wa kidhalimu. Hidaya anapendekeza kuwe na uhusiano wa kibinadamu ambao unaongozwa na akili na busara. (uk. 55).

Kuhusu swala la ndoa, Hidaya anauona ule ushahidi wa 'usafi wa kitumbua' kama kigezo cha kupimia ubora wa mwanamke wa kuoa ni maonevu dhidi ya mwanamke. Anasema kwamba hiyo si haki kwa mwanamke, kwa kuzingatia ukweli kuwa wanaume hawana ushahidi sawa na huo na wala hilo haliwafanyi kuwa 'safi kabla ya ndoa'.

**3.1.5 Wanawake kuungana kutetea maslahi yao.** Katika *Migogoro* (2006), ushirikiano wa wanawake umejadiliwa kwa mapana na marefu. Kupitia chama cha Ngao, wanawake wameshirikiana kikamilifu ili kushughulikia maslahi yao. Vijana Rukia na Farida wanawaunga mkono wanawake wenzao ili kumkaribisha mgeni na mfadhili wa chama chao. Wanafanya hivyo kwa kutunga mashairi yanayotangaza matatizo yao na kuomba msaada. Isitoshe, wanajitolea kufasiri lugha na utamaduni kwa mgeni wao Bw. Alex Taylor. Ushirikiano wao ni dhihirisho la jinsi wanavyothamini muungano wa wanawake kama hatua ya kuleta ukombozi wa mwanamke.

Vijana wana mtazamo chanya kuhusu ukombozi wa mwanamke. Jambo hili linadhihirishwa na namna wanavyofurahishwa na sifa na umaarufu wa chama cha Ngao. Farida, kwa niaba ya vijana wa kike, anadokeza kuwa wanafurahishwa na upepo unaovuma wa mabadiliko ambao bila shaka unahusishwa na ufanifu wa chama cha Ngao ambacho kusudi lake ni kutetea maslahi ya wanawake. Kwa hivyo, ni wazi kuwa vijana wa kike wana hamu na fahari kuhusu kufanikiwa na kuungwa mkono kwa chama cha ushirika cha Ngao (uk. 78).

**3.1.6 Vijana kuwa mstari wa mbele kutetea wanawake:** Katika tamthilia hii ya *Kitumbua kimeingia mchanga* (2000) kijana Fikirini ni mwanafunzi wa Chuo Kikuu na pengine masomo yake yamemsaidia kuelewa usawa unaopasa kuwa baina ya mwanamume na mwanamke. Anajitokeza kumtetea mpenziwe Hidaya dhidi ya shutuma anazolimbikiziwa na Bi. Haja na Bw. Mambo, ambao wana lengo la kumwaminisha kuwa mchumba wake ni mhuni asiyefaa kuolewa.

Kinyume na maoni ya wazee hao, Fikirini ana mtazamo chanya kuhusu ukombozi wa wanawake. Hiyo ndiyo sababu anayapuuzilia mbali maoni yao akisema kuwa

hawezi kumwacha Hidaya kwa sababu moja kuwa alionekana akiandamana na wanaume.

> Fikirini: Mimi sujui hayo... na hata nikijua; mtu hawachi kuoa mke kwa kutazama kafuatana na nani. (uk. 33).

Maoni ya Fikirini ni kuwa tatizo la ukandamizwaji wa wanawake linatokana na jamii kutotaka kutoka katika ukale, kung'ang'ania ukale katika kila kitu; ukulima, mwenendo wa jamii, utamaduni, siasa, uchumi, elimu na kadhalika. Anaongeza kwamba, kila kitu katika jamii kinaonekana kuongozwa na jinsi mababu zetu walivyokuwa wakiishi. Hata hivyo, anatoa rai kuwa pana haja ya jamii kubadilika. Anapendekeza kuwa vijana wawe mstari wa mbele kubadilisha mambo. (uk. 52).

**3.1.7 Wanawake wadai uhuru wao**. Katika tamthilia ya *Migogoro* (2006), vijana wanaona nafasi ya kwenda ng'ambo masomoni kama fursa adimu ya kufurahia uhuru wao. Wanadhani kwenda mbali na wazazi wao kutawaepusha na kudhibitiwa kwa kila namna na wazazi wao. Dhuluma kubwa wanayoichukia ni kule kubaguliwa kwa kijana wa kike hasa katika kutangamana na vijana wenzao wa kiume.

Vijana wa kike wanapojikwatua au kutembea kwa madaha wanafikiriwa kuwa na nia ya kuwavutia wanaume, ili kufanya uovu. Wanaona kuwa uonevu huo hufanyiwa vijana wa kike kuliko wa kiume. Vijana wanawalaumu wazazi wao kwa kuwadhibiti kupindukia (uk. 93).

S. Mamuya (1974:23), akizugumzia mitindo mipya inayoigwa na vijana na ambayo inawakera wazazi, alisema ya kwamba badala ya kutumia mabavu itafaa wazazi wajadiliane na watoto na kufikia uamuzi kuhusu mambo ambayo yataweza kukubalika pande zote mbili. Aliongeza kuwa itabidi wazazi nao wajaribu kuwa

na fikira za kisasa, wasipinge tu mitindo kwa vile ni mitindo mipya, bali wajaribu kuona ubaya wake na uzuri wake.

Bali na kuwa vijana wa kike wanaonewa zaidi na utamaduni, bado wanatuhakikishia kuwa kuna matumaini ya hali hiyo kubadilika.

Farida: Usijali dada. Nikitazama upeo wa macho, naona mapambazuko ya usiku huu wa dhuluma.

Rukia: Nautamani mwanga wa uhuru kwa moyo wangu wote.

Kuhusu kuchaguliwa wachumba, vijana wa kike wana maoni kuwa kuchaguliwa mchumba hakufaulishi ndoa. Mtazamo wao ni kuwa ndoa hudumu kwa misingi ya kuwa na mapenzi ya dhati wala sio kuchaguliwa mchumba na wazazi (uk. 98).

Vijana wa kike hawaoni kizuizi cha kufurahia maisha kwa kutangamana na vijana wenzao wa kiume. Wasichana na wavulana walishirikiana kuadhimisha siku ya kuzaliwa ya Farida nyumbani kwao. Walitabaruku na kucheza pamoja. Mwelekeo huu usio wa kibaguzi unadhihirika katika ule wimbo wa Rombo walioucheza Karamuni. (uk. 80). Maneno ya wimbo huo yanaashiria kuwa vijana wanastahili uhuru na uhuru wao ni uhuru wa wanawake pia.

### 3.2.0 MTAZAMO WA VIJANA WA KIUME KUHUSU UKOMBOZI WA MWANAMKE.

Kama tulivyotangulia kujadili awali, inaonekana kuwa waandishi hawa watatu wameyapatia umuhimu mkubwa mawazo ya vijana wa kike katika kuchangia ukombozi wa mwanamke kuliko vijana wa kiume. Hata hivyo, hawakukosa kugusia mtazamo wa vijana wa kiume katika kazi zao japo kwa kifupi tu.

**3.2.1 Kuwaunga mkono wanawake katika juhudi zao:** M. Mbatiah (2006) amegusia mchango wa wahusika vijana katika ukombozi wa mwanamke kama njia ya kudhihirisha mtazamo wao. Mtazamo wa wavulana unadhihirika kupitia kwa mhusika Alex Taylor. Alex Taylor ni kijana wa kimarekani ambaye ametumwa kwa niaba ya shirika la *helpline* kuleta msaada kukisaidia chama cha Ngao. Ana heshima kwa Rukia na anamtii anapomwambia mapenzi yao hayapaswi kusababisha ukosefu wa adabu kwa wazazi wake na pia kuvunja kaida na mila za jamii yake.

Hatua ya Alex kukubali matakwa ya Rukia ya kuomba ruhusa ya kuendeleza uchumba wao kwa wazazi ni ishara kuwa anaheshimu haki na usawa wa wanawake. (uk.125-128).

K.wa Mberia (1997), naye anaonyesha mtazamo huo huo wa vijana wa kiume kushirikiana na wanawake ili kuleta mabadiliko. Katika kisa cha Natala kunyang'anywa cheti cha kumiliki shamba la mumewe, mwandishi anapendekeza vita vya ukombozi visiachiwe wanawake peke yao bali hata vijana wa kiume wanapaswa kutoa mchango wao. Bala na Gane wanaonyesha ushirikiano wao na Natala katika kumpigania anaponyang'anywa cheti cha kumiliki shamba la 'marehemu' mumewe. (uk 56).

**3.2.2 Kukosa msimamo thabiti:** S. Mohamed (2000) anatufichulia udhaifu wa vijana wa kiume kuhusu swala hili. Fikirini, ingawa ana mtazamo chanya kuhusu ukombozi wa wanawake, anajikuta katika njia panda anapomtaka mpenziye Hidaya amhakikishie uaminifu wake. Fikirini anaonyesha kuchanganyikiwa kuhusu ikiwa ataongozwa na mila za jamii yake au na busara zake. Anamtaka rafiki yake amhakikishie iwapo 'kitumbua' chake amekitia mchanga kama wanavyodai wazee wake lakini anapoona swala lake linamkera mpenziwe analijutia. Fikirini anajitetea kwa kuilaumu jamii yake (uk. 52).

Hali nyingine isiyo wazi inasimuliwa katika tamthilia ya *Migogoro* (2006). Kijana wa kiume ambaye yupo kwa kutajwa na wala shughuli au mawazo yake hatujafahamishwa na mwandishi anaitwa Mwacharo bin Kiroboto. Kijana huyo amepangiwa kumwoa Rukia pindi amalizapo mtihani wake (uk.24). Ingawa hatujui mengi kuhusu mtazamo wake, tunakisia kuwa hapingi wazo hilo. Ikiwa analikubali bila maswali, basi yamkini anaunga mkono unyanyasaji wa wanawake.

**3.3.0 SABABU ZA VIJANA KUWA NA MITAZAMO HIYO.**

Tumejadili mitazamo ya vijana wa kike na wa kiume kuhusu ukombozi wa mwanamke. Tumegundua kuwa vijana wana mitazamo karibu sawa kuhusu vita vya usawa wa wanawake. Ingawa kwa jumla vijana wanaunga mkono ukombozi wa wanawake na wako radhi kuwatetea kwa hali na mali, bado msimamo wa vijana wa kiume unatetereka. Hata hivyo, kila tapo la vijana lina sababu zake kuchukua mtazamo waliouchukua kuhusu swala hilo.

**3.3.1 Elimu na ajira ni nguzo muhimu katika ukombozi:** Tumekwisha kutaja kwamba vijana wa kike wanachukulia kuwa elimu na ajira kama nguzo muhimu katika ukombozi wao. Maoni haya yamechochewa na utambuzi wa mchango wa elimu kuwafahamisha kuhusu haki zao kama binadamu wenye uwezo na haki sawa na wanaume. Vile vile, elimu itawawezesha kusomea taaluma nzuri zitakazowapatia kazi zenye kipato kizuri. Aidha, hii itakuwa mbinu ya kujikuza kiuchumi na kuepukana na tabia ya utegemezi ambayo ndiyo inayowapelekea kuteswa na kudharauliwa na wanaume. K. Mule (1991) aliafiki maoni ya wale watafiti waliomtangulia kuwa mwanamke ameonyeshwa kama kiumbe duni na mtegemezi wa mwanamume.

**3.3.2. Mila za kale zimepitwa na wakati:** Kuhusu mila na tamaduni zinazowalazimisha vijana kuchaguliwa wachumba na wazazi wao, maoni yao ni kuwa tamaduni hizo zimepitwa na wakati na tabia ya wazazi wao kuzidi kuzing'ang'ania ni sawa na kupiga ngumi ukuta.

Katika tamthilia ya *Migogoro* (2006), Farida (uk.22) anashadidia hoja hii kuwa, hakuna kizuizi chochote ambacho wazee wao wanachoweza kuuwekea wakati usibadilike. Hali kama hii ndiyo anayozungumzia E. Hussein (1971) katika Wakati Ukuta aliposema:

> "Hakuna mtu anayeweza kushindana na wakati.
> **Wakati ukuta, ukipigana nao utaumia mwenyewe.** Tutagombana na watoto wetu bure" (uk.17).
>
> (Msisitizo wetu)

**3.3.3. Haja ya kubadilika na wakati:** Katika tamthilia ya *Kitumbua kimeingia mchanga* (2000), Fikirini anatoa sababu ya mtazamo wa vijana. Anadai kuwa inabidi jamii ibadilike kufuatia jamii zingine zilivyobadilika na kwamba vijana wana jukumu la kuyaongoza mabadiliko hayo. (uk. 52); Haja ya mabadiliko pia inachochewa na elimu ya kimagharibi wanayopokea vijana, ambayo lazima iwaathiri kimawazo.

Vijana wa kiume na wa kike wanaounga mkono juhudi za kumkomboa mwanamke ni wale walio na elimu. Mfano wa vijana hao ni Rukia, Farida na Alex katika tamthilia ya *Migogoro (2006).* Hawa wana fikira za kifeministi ambazo wamezibugia pamoja na ustaarabu unaoandamana na elimu ya kimagharibi kama anavyosema E. Hussein katika *Wakati Ukuta* (1971:17) ni kwamba watoto wetu hawawezi kulaumiwa kwa mitazamo yao inayopigana na ya wazazi wao kwa

kuwa wamekwenda shuleni kusoma kizungu na sharti waige kila kitu chao kikiwemo mavazi, mila na hata tabia.

### 3.3.4 Tathmini

Katika sehemu hii tutatathmini jinsi waandishi wa tamthilia hizi tatu walivyolishughulikia swala la mitazamo ya vijana kuhusiana na ukombozi wa wanawake. Lengo letu ni kukadiria kiasi ambacho waandishi hawa walivyolipa umuhimu swala hili.

S. Mohamed (2000), katika *Kitumbua kimeingia mchanga* amelipa suala hili uzito mkubwa kupitia kwa wahusika Fikirini, Hidaya na Faki. Mwandishi huyu anadhihirisha mchango wa vijana katika kupigania uhuru na usawa wa jinsia ya kike. Amewasawiri vijana wenye elimu ya Chuo Kikuu na ambao wana ari ya kubadilika na wakati lakini juhudi zao zinakabiliwa na wazee wenye mawazo ya kihafidhina.

Mgogoro uliopo baina ya vijana na wazee katika tamthilia ya S. Mohamed (2000) unasababishwa na tofauti za kimtazamo kati ya vijana na wazee kuhusu uhuru wa vijana na hasa katika uchaguzi wa wachumba, jambo ambalo linakiuka haki na usawa wa wanawake.

Katika tamthilia ya *Migogoro* ya M. Mbatiah (2006), tofauti ya kimtazamo baina ya wazee na vijana imeshughulikiwa kupitia wahusika wa kike peke yake. Wahusika hawa ni Rukia, Fatuma na Farida. Jambo hili ni tofauti na jinsi swala hili lilivyojadiliwa kupitia wahusika wengi wa kiume kwenye tamthilia ya *Kitumbua kimeingia mchanga*. Hata hivyo, waandishi hawa wawili wamelipa uzito mkubwa suala la ukombozi wa mwanamke.

Mwandishi mwingine ambaye tumetalii kazi yake ni K.wa Mberia (1997), ambaye kazi yake imelizungumzia swala la ukombozi wa mwanamke kupitia Mgogoro uliozuka baina ya Natala na ukoo wa mumewe. Jamaa za Tango wanamnyima haki ya kurithi mali ya mumewe. Suluhisho la mzozo huo ndilo linalotupa mtazamo wa vijana ambao wanawakilishwa na Bala na Gane.

Tukilinganisha namna waandishi hawa walivyolishughulikia swala la mitazamo ya vijana kuhusu ukombozi wa mwanamke, hatutakosa kutambua mchango mkubwa alioufanya M. Mbatiah katika tamthilia ya *Migogoro.* Ameonyesha jinsi wahusika vijana wa kike wanavyojibidiisha kutafuta ukombozi wao lakini hajaonyesha mawazo ya vijana wa kiume kuhusu ukombozi wa mwanamke. Jambo hili pengine linatokana na uteuzi wake wa wahusika ambao haukuhusisha vijana wa kiume. Hata hivyo, amefaulu kuwasawiri wahusika vijana wenye mtazamo chanya kuhusu ukombozi wa mwanamke.

S. Mohamed naye katika tamthilia yake amewasawiri wahusika vijana wa kiume pamoja na wa kike. Wote hawa kwa jumla wanadhihirisha mtazamo chanya kuhusu ukombozi wa jinsia ya kike isipokuwa mhusika Fikirini ambaye msimamo wake unatetereka. Ingawa anaunga mkono ukombozi wa jinsia ya kike, anadhihirisha hofu na kuchelea lawama kutoka kwa wazee wake na jamii kwa jumla.

Kama alivyofanya M. Mbatiah katika kazi yake, K. wa Mberia naye hakuwakuza vyema wahusika vijana wa kiume ili kubainisha waziwazi mitazamo yao juu ya swala husika. Kwa jumla mitazamo ya vijana hawa, wawe wa kike au wa kiume inafanana. Wote wanaunga mkono ukombozi wa mwanamke. Sababu wanazotoa kwa kuchukua msimamo huo wa kimapinduzi ni kuwa, kwanza, jamii nyingi za ulimwengu zimebadilika na hivyo inabidi kila mmoja abadilike na wakati. Pili, wanashikilia kuwa mabadiliko ya aina hii lazima yaongozwe na vijana. Tatu,

vijana waliosoma hawaoni haja ya kuendelea kukumbatia baadhi ya mila na desturi kandamizi na ambazo zimepitwa na wakati.

### 3.3.5. Hitimisho

Katika sehemu hii ya tatu tumejadili mitazamo ya vijana kuhusu ukombozi wa mwanamke. Tumegawa vijana katika makundi mawili ambayo ni vijana wa kike na wa kiume. Tumeutumia mgao huo kwa kuzingatia kuwa mitazamo ya vijana wa jinsia hizi mbili inatofautiana hata ingawa kwa kiwango kikubwa inafanana.

Ili kukabiliana na dhuluma ambazo zinaelekea kuwa zimehalalishwa na utamaduni na mila za jamii wanamoishi wanawake, vijana wa kike wameamua kutumia elimu kama msingi wa ukombozi wao. Kulingana na maoni yao, elimu bora itawapa kazi nzuri ambayo itakuwa kivuko cha kutoka katika umaskini kama alivyodokeza M. Mbatiah katika tamthilia ya *Migogoro,* kuwa umaskini na ukosefu wa elimu ndio kikwazo kikubwa kwa ukombozi wa mwanamke.

Ushirikiano baina ya vijana wa kike na wa kiume umetambuliwa kuwa nguzo muhimu katika harakati za kupigania ukombozi wa mwanamke. Vijana wa kike wamedhihirisha nia yao kushirikiana na wenzao ili kufanikisha azima yao. Katika tamthilia ya *Natala* (1997), Gane na Bala wanashirikiana na Natala kumtetea anapodhulumiwa haki yake.

Ili kushinda katika vita dhidi ya unyanyasaji wa jinsia ya kike, vijana wa kike wanapendekeza kila mwanamke asimame kidete kutetea heshima yake binafsi na ya wanawake kwa jumla.

Vijana wa kiume nao, mbali na kuwaunga mkono wenzao wa kike katika ukombozi wao, wanathamini sana juhudi za pamoja kupinga ukale. Wanaamini mila na tamaduni kandamizi hazina nafasi katika ulimwengu unaobadilika na

kuthamini haki na usawa wa kila mmoja. Sababu wanazotoa wote ni kuwa kuendelea kuzing'ang'ania ni sawa na kupiga ngumi ukuta.

Ingawa tumeonyesha kuwa mitazamo ya vijana wa kike na wa kiume ni sawa kuhusu ukombozi wa mwanamke, pia ni muhimu kutaja kuwa vijana wa kiume hawana msimamo thabiti kuhusu swala hili. Baadhi yao wanadhihirisha kuathiriwa na mawazo ya wazee wao na wanachelea kuwavunja moyo au kulaumiwa na jamii yao.

# SURA YA NNE

## MITAZAMO YA WAZEE WA KIKE NA WA KIUME KUHUSU UKOMBOZI WA MWANAMKE.

### 4.1.0 MITAZAMO YA WAZEE WA KIKE

#### 4.1.1 Utangulizi

Katika sura hii tutaangazia namna ambavyo wazee wanavyolipokea suala la ukombozi wa mwanamke. Mtazamo wa wazee wa kike na wa kiume unatarajiwa kuwa sawa ukilinganishwa na wa vijana hasa kuhusu swala linalohusika. Hata hivyo, kati ya wazee hao pana uwezekano kuwa na tofauti za kimtazamo baina ya wazee wa kike na wazee wa kiume. Hiyo ndiyo sababu inayotuchochea kuchunguza maoni ya kila kundi la wazee peke yake.

Katika sura hii, kwanza tunachunguza mitazamo ya wazee wa kike na kisha wa wazee wa kiume kuhusu swala la wanawake kwenye tamthilia hizi tatu. Kama tutakavyoona baadaye, katika utafiti huu, pana uwezekano kuwa wanawake wazee ndio wanaochelewesha ukombozi wa mwanamke kwa kushirikiana na wanaume kuwanyanyasa wanawake wenzao.

#### 4.1.2 Mwanamke anastahili kudhibitiwa tangu utotoni

Katika tamthilia ya *Kitumbua kimeingia mchanga* (2000), mwandishi anatufichulia maoni ya Bi.Sikitu kuhusu malezi ya mtoto wa kike. Anadokeza katika (uk. 11) kuwa msichana anafaa kulindwa vilivyo ili asiharibiwe na wanaume. Akitumia jazanda ya kifaranga na mwewe ili kusisitiza uhusiano uliopo baina ya wasichana na wavulana, anaonyesha mawazo yake kuhusu uhuru wa mwanamke yalivyo. Mshabaha huu wake una dhamira ya kuonyesha kuwa mwanamke anastahili kudhibitiwa angali mchanga ili asiharibike.

Ingawa ni jambo la busara kuhakikisha watoto wa kike wamelelewa kwa uadilifu, kwa upande mwingine hali hii ikizidishwa inaweza kumfanya mtoto wa kike kuishi kama mtumwa. Kama anavyosema mhusika Bi. Tukaije, katika (uk. 12), mtoto wa kike akitaka kuharibika, ataharibika tu hata atiwe gerezani na kufungwa silisili. Anachoelekea kumaanisha mwandishi huyu ni kuwa haiwezekani kumlea mtoto wa kike kwa kumdhibiti katika kila hali, bali kinachofaa ni uhuru wa kadiri.

**4.1.3 Mahali pa mwanamke ni jikoni**: Katika tamthilia ya *Kitumbua kimeingia mchanga* (2000), Bi.Sikitu anawakilisha maoni ya wanawake wazee kwamba mwanamke anafaa kuwatumikia wenzake wa kiume katika kazi za nyumbani. Hali hii inajitokeza tena katika (uk. 8) ambapo Bi.Sikitu anamwagiza bintiye Fatuma kuwatayarishia chakula nduguze na babake ambao wamekwenda msikitini kusali. Jambo kama hili linarejelewa tena na mwandishi katika maelezo ya utangulizi kwenye onyesho la pili. Hapa, Fatuma na Bi. Sikitu wanajishughulisha na kuandaa vyakula mezani huku wanaume, yaani Bw. Mambo, Fikirini na Faki wakisoma.

Tabia hii ya Bi. Sikitu inawakilisha mtazamo wa wanawake wazee ambao huwahimiza watoto wa kike kujishughulisha na kazi za jikoni badala ya kusoma kama wenzao wa kiume. Labda hali hii huwafanya watoto wa kike kuhisi kuwa wao si sawa na wenzao wa kiume. Hali kama hii inawafunza watoto wa kike kuwatumikia na kuwanyenyekea wanaume; jambo ambalo tunafikiri ndilo linalochangia kudunishwa kwa wanawake.

**4.1.4 Kuwadharau na kuwaumbua binti zao:**Kumdharau mtu ni kumwona kama asiyefaa kamwe. Wazee wa kike, kama wanavyosawiriwa na Mohamed S. wana tabia ya kuwadharau na kuwaumbua binti zao. Hali kama hii huwavunja moyo na kuwafanya wajione kama wasio na thamani wakijilinganisha na wenzao wa kiume. Mfano mzuri hapa unawakilishwa na mawazo ya Bi. Sikitu na Bi. Mwatima kuhusu Hidaya ambaye ni mpenzi wa Fikirini.

Wanayasema mengi ya kumuumbua wakikusudia kumvunja moyo Fikirini ili akubali ushawishi wao kuvunja uchumba wake na Hidaya. Wanamdharau na kumuumbua Hidaya katika dondoo hili:

Bi. Mwatima: Mambo si hayo... Nimekuta hicho ki-Hidaya... mnh; a-a. [Anapiga kofi] Dunia imeharibika. Shoti anapita akicharaza njiani, kahanikiza sauti, kifua mbele, madodo pwa-pwa-pwa yasiyotiwa mbele, madodo pwa-pwa-pwa yasiyotiwa vikapuni... [Anasimama kwa kupepesuka kumwiga Hidaya alivyokuwa akienda huku madodo yakidunda; kisha anarudi kuketi pale pale sofani] katiwa ngosho na kundi la wanaume... wengine huku, utadhani malkia wa laana... mtoto keshaonja, tamu imemnogea. Lo! Vitoto vinaanza mambo vingali vikambaa. Maskini mama yake...nani atakayechukua ugonjwa ule kuutia ndani mwake? Ama kweli Hidaya haikuwa hidaya tena! Bi. Sikitu! Ki-Hidaya gani hicho bibi kisichokoga kikatakata? [Akimtazama mwanawe Fikirini ambaye anaangusha uso chini]

Bi. Mwatima: Huyu wa Bi.Tiba madongoporomoka!

Bi. Sikitu: Aaa, unashangaa nini na nyumba nzima mashetani...(uk.19-20).

**4.1.5 Lazima mila kuheshimiwa:** Wanawake wazee wanajiona kama watetezi wa mila na desturi za kale. Mila wanazodai kuzitetea zinawakandamiza wanawake. Bi. Sikitu amechorwa kama mhusika anayeshikilia mila za kale zinazomtaka msichana kuwa bikira kabla ya ndoa. Hiyo ndiyo sababu anafadhaishwa na arusi ya Baddi na Zubeda ilipokosa kuridhisha matarajio yao. Sababu ilikuwa 'kitumbua' kilikuwa kimeingia mchanga. Anaionea aibu arusi ya vijana hao kwa sababu ya kutotimiza masharti ya mila yao. Tunachukulia mtazamo huu wa wanawake wazee kama kikwazo kwa ukombozi wa mwanamke.

Hali hii ya kupenda kutimiza matakwa ya mila huku wakipuuza haki za wanawake inajitokeza tena katika tamthilia ya *Natala* (1997). Mama Lime akitoa sababu za kuhitilafiana kwake na Natala, anadai kuwa kitendo cha Natala kukataa kumtii na

kutii mila ya kurithiwa au kuolewa na Wakene ambaye ni ndugu wa 'marehemu' mumewe ni ukosefu wa adabu.Mama Lime anakazania kwamba Natala anavunja matarajio ya ukoo wa marehemu mumewe. Anasema kuwa matarajio ya ukoo wao yana msingi wa mila na kwa hivyo ni lazima Natala ayafuate.

**4.1.6 Uhuru wa kuvaa:** Katika tamthilia ya *Migogoro* (2006), mwandishi anamsawiri mhusika Amina akiwa na mtazamo chanya kuhusu uhuru wa wanawake wa kimavazi. Amina ana maoni kuwa kuwadhibiti wasichana sana hakusaidii. Anataja mfano wa bintiye Kadogo ambaye alifariki kwa ugonjwa. Anajuta kwa kumuunga mkono babake katika ulezi wa binti yao. Baba Kadogo akiwa mhubiri alipenda bintiye afuate mfano wake wa uadilifu.

Kadogo alitaka aruhusiwe avae nguo fupi kama wasichana wengine wa rika lake lakini babake akamkataza kwa madai kwamba nguo hiyo ingemfanya aanze kutamaniwa na wanaume, jambo ambalo lilipingana na ukristo wake. Kwa jumla maoni ya Amina ni kuwa mwanamke anastahili uhuru wake hasa anapotimu miaka kumi na nane ambapo huwa anaweza kujiamulia kuhusu maisha yake. Maoni haya ya Amina yanatuelekeza kwenye mtazamo wake kuhusu suala la wanawake.

> Amina: Namaanisha kwamba labda tulizidisha dawa ya nidhamu.
> Wajua dawa hutibu ukinywa kipimo chake. Ukizidisha, inadhuru
> badala ya kutibu.
>
> Hamisi: Kile wazungu wanachoita *overdose*(uk. 58).

Maoni ya Amina yanaungwa mkono na Hamisi. Mtazamo wa Hamisi kuhusu mavazi ya wanawake ni kuwa, wanawake wanafaa waruhusiwe kuvaa wapendavyo. Hamisi anatoa mfano wa bintiye Rukia. Anasema kuwa alimruhusu kuvaa apendavyo baada ya kugundua wasichana wenzake hupenda kuvaa hivyo. Maneno haya yake yanaonyesha kuwa Hamisi ni miongoni mwa wazee

wanaoruhusu mabadiliko na kuamini kuwa malezi yao yalikuwa tofauti na ya vijana wao siku hizi (uk. 56).

Amina ni mwanamke mzee aliye na msimamo tofauti na wa nduguye Mambo kuhusu uhuru wa mwanamke. Amina anamkashifu Mambo kwa kueneza uvumi kuwa Fatuma mkewe Hamisi ameunda na kuongoza chama ambacho nia yake ni kuzalisha migogoro baina ya wanawake na wanaume. Mambo anaunga mkono ukandamizaji wa wanawake. Jambo hili linasisitizwa na Hamisi katika uk. 60 anaposema kuwa Mambo ndiye aliyechangia kuvunjika kwa ndoa yake ya kwanza kwa kumtesa mkewe.

**4.1.7 Taasubi ya kiume:** Hii ni hali ambapo watu fulani hupendelea wanaume na kuwapuuza wanawake. Mama Lime anadhihirisha mapendeleo makubwa kwa jinsia ya kiume. Nia yake ya kuunga mkono matakwa ya ukoo wao kumlazimisha Natala akubali kuolewa kama mke wa pili na ndugu ya mumewe ni ithibati tosha kuwa hajali uhuru wa mwanamke na anaunga mkono mila zinazomruhusu mwanamume kumkandamiza mwanamke.

Kulingana na mawazo ya mama Lime, mahali pa mwanamke ni nyumbani. Hili linadhihirishwa na kifungu kifuatacho:

> Mama Lime: Kwani furaha ya mwanamke ni nini?
> Ni kuwa na makazi, kula na kushiba,
> Kuvaa nguo na kupata watoto. (uk.39).

Taasubi hii inadhihirishwa na mtazamo wa mzee Palipali na Mama Lime. Hawa wana mtazamo sawa kuhusu uhuru wa mwanamke. Mtazamo wao unaonekana wazi wanapomhimiza Wakene kumnyang'anya Natala haki yake. Mama Lime anamhimiza wakene kumtia adabu Natala baada ya kugundua kuwa Natala amekataa katakata kukubali matakwa yao. Mzee Palipali naye anawakanya Gane

na Bala dhidi ya kuingilia mzozo huo kwa madai kuwa unahusu maswala ya nyumbani. Mtazamo wa Mama Lime wa kitaasubi unawakilisha mawazo ya wanawake wengi ulimwenguni kama anavyodai mtaalamu A. Nyerges (1962:14). Akigusia tabia ya wanawake wengi wa taifa la Hungary, anasema kuwa:

> Idadi kubwa ya wanawake wanaendelea kuamini na kuendeleza imani ya jamii yao kuwa, mwanamke ana hadhi ndogo kuliko mwanamume na mahali pake ni nyumbani. (Tafsiri yetu).

## 4.2.0 MTAZAMO WA WAZEE WA KIUME

Kama tulivyotangulia kusema, mitazamo ya wazee ni tofauti. Hiyo ndiyo sababu tumewagawa katika makundi mawili ili kulishughulikia kila moja kwa zamu. Hapa tutachunguza mtazamo wa wazee wa kiume kuhusu swala la wanawake.

**4.2.1 Utukufu wa nasaba na uchumi:** Katika tamthilia ya *Kitumbua kimeingia mchanga* (2000), mwandishi hakuwasawiri wahusika wazee wa kiume na wa kike wakihitilafiana pakubwa kimtazamo juu ya ukombozi wa mwanamke. Wote wanaelekea kukubaliana kuwa, nasaba na hali ya kiuchumi ya wazazi wa mwanamke ni kigezo muhimu kinachofaa kuzingatiwa wakati wa kutafuta mchumba. Hili ndilo analosisitiza Bw. Mambo kwa mtoto wake Fikirini. Anatumia kigezo hicho kumkatalia mwanawe mchumba wake aliyejichagulia. Anadai kuwa Hidaya amezaliwa kutokana na ukoo usio maarufu na wa kimaskini. Dondoo hili linafafanua mawazo yake:

> Bw. Mambo: Alaa, hili ndilo jibu la kile kitendawili cha kitumbua kilichoingia mchanga lakini hebu twambie Bi. Mkubwa; bali na kwamba Hidaya ni mtoto wa kimasikini na ukoo wake hauna mashiko; kitu gani....(uk. 26)

**4.2.2 Lazima mila kudumishwa.** Katika tamthilia ya *Migogoro* (2006), mtazamo wa wazee wa kiume tanaupata kupitia mazungumzo ya Rukia na Farida. Farida anachukua nafasi ya Baba Farida. Majadiliano yao yanadhihirisha jinsi wazee wanavyong'ang'ania kudumisha utamaduni pasipo kutambua kuwa hali ya maisha imebadilika. Dondoo hili linadhihirisha hayo:

> Farida: [ Anaangua kicheko. Anacheka akipiga hatua kuikaribia hadhira. Kisha anasimama mbele yake na kuanza kuhutubu] Walimwengu tegeni maskio msikie vioja. Wanaoishi jana hawataki kupambazuke. Badala ya kukaribisha machweo kwa furaha, wanayalaani… (uk.22).

Wazee wa kiume wanathamini sana mila za kuwachagulia wanawake wachumba. Farida anashauriwa na 'Babake' kutokuwa na mwanaume mwingine yeyote mbali na Mwacharo bin Kiroboto ambaye amekwisha kuchaguliwa na wazazi wake kitambo ili awe mume wake. (Uk.24) babake anatoa sababu kuwa mwacha mila ni mtumwa. Kwa hivyo, mtazamo wao kuhusu uhuru wa mwanamke ni kuwa wanawake hawana uhuru wa kujichagulia wachumba.

**4.2.3 Haja ya kuwaelewa vijana:**

Bw. Nia ndiye mzee wa pekee katika tamthilia hii ya S. Mohammed (2000) ambaye anaelekea kuyaelewa matatizo ya vijana. Kwa hakika Bw. Nia anasadiki kuwa si wazee wengi wanaojaribu kuwaelewa vijana kama yeye.

Kuhusu tabia ya wazee kung'ang'ania mila zisizofaa na ambazo zimechakaa, anasema kuwa wazee hudhani ni jukumu lao kuzilinda kwa kila hali. Aidha, Bw. Nia ndiye anayetupa suluhisho la tofauti za kimtazamo baina ya wazee na vijana. Anahoji kuwa vijana wanapaswa kukubali kuwa kuna tatizo na kwamba si rahisi kusuluhisha tatizo linaloambatana na silika na desturi za watu. Vile vile, anashauri wazee wenzake waliotambua umuhimu wa kuwaelewa vijana kuwaelimisha wenzao kuhusu jambo hilo.

Bw. Nia: La muhimu kwanza, vijana mkubali kushiriki kuyatatua... na kuyatatua matatizo yanayoambatana na silka na desturi si rahisi hata chembe... Na sisi wazee tuliokwishatambua ukweli wa mambo lazima tuwashawishi wazee wengi wanaong'ang'ania kuhifadhi mambo... (uk 42).

**4.2.4 Kuheshimu haki na uhuru wa vijana.** Katika tamthilia ya *Kitumbua kimeingia mchanga* (2000), Bw. Nia anawakilisha wazee wachache ambao wameona mwanga ambao vijana wanataka kuuleta katika jamii.Anawakilisha jamii ya wazee wachache ambao wanathamini uhuru wa vijana wa kike kujiamulia maisha yao. Ametambua kuwa kuendelea kupingana na wakati hakutawazalia wazee matunda bali matokeo yao yatakuwa ni majuto.

Bali na Bw. Nia, yupo Baba Hidaya ambaye maoni yake ni kuwa hali hii ya wazee kuendelea kung'ang'ania mila na desturi za kale za kumtaka mwanamke awe bikira hadi anapoolewa zinawaaibisha wazazi. Anakubali kuwa hayo ni makosa ambavyo wazee wanastahili wajutishwe na aibu inayowafika wakati mambo yanapokwenda kinyume na matarajio yao. Alisisitiza hivi:

Baba – Hidaya : Haya ni makosa yetu sisi wazee!
Kwa nini tunaendeleza kitiba hichi
cha kuzisasambura siri za watoto wetu? (uk.63).

Katika tamthilia ya *Migogoro* (2006), Mzee Balu ndiye wa pekee ambaye anatetea maslahi ya wanawake. Anawashauri jamaa zake kuheshimu hisia za Natala. Kwanza, kama mwanamke na pili, kama mke wa 'marehemu'. Hatua hii yake inaonyesha yuko tayari kuwapigania wanawake dhidi ya dhuluma zinazowakabili katika jamii yao. Anathamini uhuru wa Natala kuamua kuhusu mazishi ya mumewe. Anafanikiwa kuwatetea wanawake ingawa anakabiliwa na upinzani kutoka kwa jamaa zake wengine.

## 4.3.0 SABABU ZA KUWA NA MITAZAMO HIYO

Ingawa tumeonyesha kwamba kuna tofauti za kimtazamo baina ya wazee wa kike na wa kiume katika tamthilia hizi tatu kuhusu ukombozi wa mwanamke, makundi haya mawili yanaelekea kukubaliana katika maswala fulani maalumu. Hata hivyo, pale wanapokubaliana au kutofautiana wanatoa sababu za kufanya hivyo. Katika sehemu hii. tutamulika sababu za kila kundi kuchukua mtazamo waliouchukua.

**4.3.1 Jukumu la kulinda mila na desturi za kale:** Ingawa kuna tofauti za kimtazamo baina yao, baadhi ya wazee wanakubaliana kuwa wana jukumu la kuhakikisha kuwa vijana wao wa kiume na wa kike wamezifuata mila zao kikamilifu. Tukirejelea mada ya uchaguzi wa wachumba, wazee wanasisitiza kuwa ni muhimu vijana wakubali wachaguliwe wachumba na wazazi wao. Isitoshe, wazee wanaonyesha nia yao ya kutokubali mabadiliko ya kiwakati. Hata hivyo, wapo wazee wachache kama alivyo
Bw. Nia wa *Kitumbua kimeingia mchanga* (2000) ambaye mtazamo wake unahitilafiana na wa wazee wengine.

Bw. Nia anaunga mkono uhuru wa vijana na wanawake. Anashadidia kuwa wazee wanapaswa kuongozwa na dhati ya mambo kuliko kufuata fikira na hisia zao tu. Anachomaanisha mzee huyu ni kuwa; wazee wenzake hawapaswi kufumbia macho mabadiliko ya wakati na pia wasadiki kuwa wakati waliolelewa ni tofauti na wa watoto wao. Aidha, anakubali kuwa kijana yeyote awe wa kike au wakiume hatimaye huwa mtu mzima na anahitaji uhuru wake wa kujichagulia maisha atakayo.

Katika tamthilia ya *Migogoro* (2006), Mambo anasawiriwa kama mhusika asiye heshimu haki za wanawake. Tabia hii yake inatokana na utashi wake wa kujitwika mamlaka ya kuwa mlinzi wa mila na desturi za kijadi. Katika (uk.52), anasema

kwamba mila na desturi zao zinasema kuwa mume anapaswa kuwa kiongozi wa nyumba naye mkewe awe mfuasi.

Hamisi anahitilafiana na Mambo kuhusu ukombozi wa mwanamke. Hamisi anasema ya kuwa, ingawa anaheshimu mila na desturi za kikwao, hawezi kukubali kuwa mtumwa wa mila na desturi zinazomkandamiza mwanamke. Anaamini kuwa katika maisha ya leo, ndoa haipaswi kuwa na kiongozi wala mfuasi bali mke na mume wanapaswa kuwa wakisaidiana katika kulea na kuendesha nyumba. (uk.52).

Hamisi pia ana sababu zake za kuunga mkono ukombozi wa wanawake. Sababu zake zinatokana na imani yake kuwa zama za mababu zao maisha yalikuwa bahari shwari na kwamba wakati huo mila na desturi ziliyajibu maswali yote ya maisha. Anaendelea kusema kuwa maisha ya leo ni bahari iliyochafuka na kwamba mawimbi yake ni makubwa kiasi kwamba mtu asipokuwa mwangalifu atazama. Kwa hivyo, maoni yake ni kwamba majibu ya zamani hayafai kwa maswali ya leo. Kwa jumla anashikilia kuwa mila fulani zapaswa kutupiliwa mbali kwa kuwa zimepitwa na wakati (uk. 53). Mtazamo wa Hamisi ni kuwa tamaduni za jadi zinazomkandamiza mwanamke zinastahili kuangaliwa kwa jicho la kiuhakiki.

**4.3.2 Wanawake na siasa:** Katika tamthilia ya *Migogoro* (2006) mhusika Mambo anapinga juhudi za wanawake kushiriki katika siasa. Anatahadharisha kuwa, kwa mwanamke kuingia siasani ni sawa na kujitosa kwenye mzinga wa nyuki wakali bila kuchukua kinga cha moto. Ingawa anayetahadharishwa ni Fatuma ambaye hana nia ya kujiunga na siasa, mtazamo huu wake unawanyima wanawake nafasi ya kutetea maslahi yao katika Bunge. Ili kupata uhuru wao, wanawake wanastahili kuwania viti vya ubunge kama hatua ya kujipigania. Siasa itawawezesha kushiriki katika uundaji wa katiba na kuondoa baadhi ya sheria zinazowakandamiza wanawake.

### 4.3.3 Elimu kama msingi wa ukombozi:

Katika tamthilia ya *Migogoro* (2006), Fatuma anasawiriwa kama mhusika anayethamini elimu kwa mwanamke. Anasadiki kuwa wanawake wanahitaji elimu na uhuru wa kufanya kozi wazipendazo pasipo kushinikizwa na wazazi wao wasomee taaluma wasizozipenda. Hii ndiyo sababu anamshauri mumewe asijaribu kupinga mpango wa binti yao wa kusomea taaluma ya uuguzi huko Marekani pindi afanikiwapo kupata ufadhili wa kimasomo kutoka kwa serikali (uk. 81).

Mawazo haya ya Fatuma yana ukweli kwa kiasi fulani lakini kama anavyosema mtaalamu A. Nyerges (1962:16), elimu peke yake haitoshi kumhakikishia mwanamke uhuru wake. Anadai kuwa haki ya kufanya kazi na elimu haikutosha kumpa mwanamke wa ki-Hungary ukombozi aliohitaji. Kutojimudu kwa mwanamke kiuchumi ndiko kulikochangia pakubwa kwa wanawake wengi wa Hungary kuwa na hadhi ya chini.

Mawazo ya mtaalamu A. Nyerges (1962) yanaoana kwa kiasi fulani na yale ya G. Ozkaya (1981) ambaye anasema ya kwamba mwanamke ameendelea kuwa mtumwa kimwili na kiakili. Sababu kuu ya mwanamke kuwa katika hali hii kulingana na mtaalamu huyu, inatokana na tabia yake ya kuwa mtegemezi wakati wote.

G. Ozkaya (1981) anaendelea kusema kuwa mwanamke kupata haki ya kielimu, kiuchumi na kisheria ni hatua muhimu kuelekea ukombozi wake katika jamii. Hata hivyo, ikiwa wanawake wote hawatafanikiwa kupata haki hizi basi, itakuwa vigumu kuzungumzia ukombozi wa mwanamke katika jamii hiyo.

## 4.4.0 KULINGANISHA MITAZAMO YA VIJANA NA WAZEE

Sura hii itajishughulisha na ulinganishaji wa mitazamo ya vijana na wazee kuhusu ukombozi wa mwanamke kwa mujibu wa matokeo ya utafiti huu. Aidha, tunajadili matokeo ya utafiti wetu kulingana na madhumuni yake kama yalivyodhihirika katika uchanganuzi wa vitabu vilivyoshughulikiwa. Vile vile, katika sura hii tutahitimisha kwa kubainisha matokeo ya utafiti pamoja na kutoa mapendekezo kuhusu tafiti za baadaye katika kazi za fasihi.

Katika utafiti huu imebainika kuwa suala la ukombozi wa wanawake limezua mitazamo mbalimbali baina ya vijana na wazee. Vile vile, miongoni mwa vijana kumeibuka tofauti za kimtazamo baina ya vijana wa kike na wa kiume. Hali kadhalika, miongoni mwa wazee wa kike na wa kiume kuna mitazamo inayohitilafiana. Hata hivyo, katika sehemu hii tutalinganisha mitazamo ya makundi haya mawili bila kujali jinsia zao.

Ushirikiano wa vijana wa kike na kiume umetambuliwa kuwa nguzo muhimu katika kushinda vita dhidi ya udhalimu kwa wanawake. Vijana wanaongozwa na imani kuwa, ikiwa ushindi utapatikana ni lazima uhusishe juhudi za pamoja miongoni mwa vijana bila kujali jinsia zao. Mbali na ushirika wa vijana, wanawake nao wana jukumu la kuungana na kuunda chama chao cha kutetea haki na usawa wao. Chama cha wanawake kinachowaleta pamoja ili kuanzisha mikakati ya kusaidiana kujiinua kiuchumi. Mtazamo huu wa vijana unatokana na utambuzi wao kuwa sababu kuu ya wanawake kudhulumiwa inatokana na hali yao ya utegemezi.

Vijana pia wana maoni kuwa ukombozi wa mwanamke unatokana na mwanamke mwenyewe kuamua kusimama kidete kutetea heshima yake binafsi na ya wanawake kwa jumla. Mtazamo huu wao unatokana na kuamini kuwa mwanamke

anapojiachilia na kujinyenyekeza kwa mwanamume atadharauliwa na kutumiwa vibaya.

Wazee nao kwa upande mwingine, wanaongozwa na mawazo ya kitaasubi. Wengi wao hupendelea mtoto wa kiume na kumpuuza wa kike. Jambo hili ndilo linalowapelekea kuwasomesha wavulana na kuwanyima elimu wasichana. Vile vile, wazee wanashikilia kuwa wanawake wanafaa kudhibitiwa wangali wachanga ili kuhakikisha hawatasababisha mgogoro baadaye katika ndoa wakidai haki na uhuru wao.

Ni maoni ya wazee kuwa; mwanamke wa kuoa anafaa atokane na ukoo mtukufu kimaadili na kiuchumi. Vinginevyo msichana anayetokana na nasaba duni hastahili kuolewa. Mtazamo huu wa wazee ni wa kibaguzi na ni dhuluma kwa wanawake. Pamoja na kwamba wazee wengi wana mtazamo hasi kuhusu ukombozi wa mwanamke, bado kuna wazee wachache ambao wameelewa umuhimu wa kubadilika na wakati. Wazee hao wachache ndio wanaotupa matumaini kuwa siku zijazo huenda wazee wakabadilisha mtazamo wao.

Taasisi ya ndoa na utamaduni zimetambuliwa kama chanzo kikuu cha tofauti za kimtazamo baina ya vijana na wazee katika kazi zilizohakikiwa. Imebainika kuwa vijana wanapendelea kubadilishwa kwa mila na desturi zinazowataka wazee kuwachagulia binti zao wachumba, kuwa bikira kabla ya ndoa na urithi wa wajane. Vijana wanashikilia kuwa tamaduni hizi zinaonea mwanamke huku zikimpendelea mwanamume na kwa hivyo zinafaa zitupiliwe mbali.

Kwa upande wa wazee, mtazamo wao ni kuwa hali inafaa kubakia kama ilivyokuwa wakati wa mababu. Wakitumia msemo wa ‘Mwacha mila ni mtumwa’ wanaelekea kupuuza haki na uhuru wa wanawake pasipo kujali hisia zao.

Wazee wangali wanahimiza mila zidumishwe hasa zinazohusu mavazi, uchumba, urithi wa wajane na ubikira wa wanawake. Mila hizi ni kandamizi na ndizo zinazosababisha mgogoro mkubwa baina ya vijana na wazee.

Mbali na kwamba vijana na wazee wanahitilafiana kimtazamo juu ya mambo kadhaa kama hayo tuliyoyajadili hapo juu, bado wanaelekea kuafikiana katika mengine. Jambo moja ambalo wazee na vijana wanakubaliana ni kuhusu elimu. Wazee na vijana wanakubaliana kwa kauli moja kuwa elimu kwa wanawake ni nguzo muhimu katika kuleta mabadiliko yatakayopelekea ukombozi wa wanawake miongoni mwa jamii. Wote wanadai kuwa elimu humsaidia mwanamke kupata ajira ambayo humpa nguvu za kiuchumi. Mwanamke aliyejikomboa kiuchumi huepukana na tabia ya utegemezi ambayo ndiyo inayomfanya kunyanyaswa na mwanamume. Elimu pia inamwezesha mwanamke kujikomboa kimawazo na kujielewa zaidi ili kuweza kudai haki na uhuru wake. Elimu sio muhimu tu kwa mwanamke bali pia kwa mwanamume kwa sababu mwanamume aliyesoma ataelewa usawa uliopo baina yake na mwanamke.

**4.4.1 Hitimisho**

Katika sura hii tumejadili mitazamo ya wazee wa kiume na wa kike. Tumetambua kwamba mitazamo yao kuhusu uhuru wa mwanamke inafanana na vile vile kutofautiana katika vipengele mbalimbali.Vile vile, tumeangazia sababu mbalimbali zinazowapelekea kuchukua misimamo waliyochukua juu ya swala husika. Aidha, tumelinganisha mitazamo ya vijana na wazee.

Katika tamthilia hizi tatu, wazee wa kike wanaonyesha kuunga mkono ukandamizwaji wa wanawake. Jambo hili linatokana na mapendekezo yao kuwa mwanamke anafaa kudhibitiwa tangu utotoni mwake. Vile vile, wanaendeleza imani ya jamii zao kuhusu majukumu na hadhi ya mwanamke katika jamii. Jamii nyingi zinaelekea kukubaliana kuwa mahali pa mwanamke ni nyumbani na wala

hapaswi kuchukua majukumu mengine nje ya jikoni. Imani hii inapaliliwa na kuendelezwa na wanawake wazee. Imedhihirika pia kuwa wanawake wazee wako mstari wa mbele kuwadharau na kuwaumbua wanawake wenzao.

Ingawa tumesema kwamba mtazamo wa wazee wa kiume na wa kike sio tofauti sana, wazee wa kiume wana maoni yao tofauti na wale wa kike. Kwa mfano, wanaume wazee wanapendelea sana uchaguzi wa mwanamke wa kuolewa utegemezwe katika utukufu wa ukoo wa binti na vile vile hali yao ya kiuchumi iwe ni kigezo muhimu. Kwa maoni yao, ikiwa msichana ametoka katika nasaba isiyojiweza kiuchumi, basi thamani yake imepungua.

Kwa upande mwingine, kuna baadhi ya wazee wa kiume ambao wameonyesha kuunga mkono ukombozi wa wanawake. Wazee hawa wanapendekeza kuwe na mabadiliko katika jinsi wazee wanavyohusiana na vijana wao. Wanapendekeza haja ya kuwaelewa vijana kwa kuzingatia kuwa wanaishi kipindi tofauti na kile walicholelewa wao.

Wazee wa kike na wa kiume wanakubaliana kuwa lazima mila na desturi za kale zidumishwe. Wanajitwika jukumu la kuwa walinzi wa mila na hawangependa kuona vijana wakizivunja. Wanachukulia kuwa uvunjaji wa mila ni kama ukosefu wa heshima kwa wazazi. Kipengele kingine ambacho wazee hawa wanachokubaliana ni kuhusu mavazi ya vijana wa kike. Wanasema kuwa vijana wa kike waruhusiwe kuvaa wapendavyo ilmradi wanadumisha adabu inayostahili. Wanaamua kufanya hivyo baada ya kutambua kuwa kuendelea kuwapinga kunazua mtafaruku baina yao na mwishowe wazazi ndio hupoteza.

Sababu za wazee kuchukua mtazamo hasi kuhusu ukombozi wa mwanamke zinatokana na uhafidhina wao. Hawapendi kuwe na mabadiliko kuhusu mila zinazomkandamiza mwanamke. Kuhusu haja ya wanawake kujiunga na siasa,

wazee wanaonelea kuwa wanawake wakijiingiza katika siasa watawatawala wanaume wao. Kwa hivyo, wanasema wanawake wenye nia ya kuungana pamoja na kuelimishana kuhusu haki zao wanastahili kukomeshwa mapema.

# SURA YA TANO

# HITIMISHO

## 5.0 Utangulizi

Sura hii imejishughulisha na mjadala juu ya matokeo ya utafiti wetu kulingana na madhumuni yake kama yalivyodhihirika katika uchanganuzi wa vitabu vilivyoshughulikiwa .

## 5.1 Muhtasari wa matokeo ya utafiti

Imedhirika katika utafiti huu kuwa baadhi ya wahusika wazee katika tamthilia tulizozihakiki hawajatambua umuhimu wa uhuru wa wanawake. Maombi yao ni kuwa mwanamke anachukua nafasi ya pili baada ya mwanamume na kwamba hali hii inapaswa kubakia ilivyo kwa kuwa inafungamana na utamaduni.

Ingawa imebainika kuwa wazee wengi ni wahafidhina, ni bora kudai kuwa wamedhihirisha mgawanyiko wa kimtazamo kuhusu suala hili. Kuna kundi Fulani la wazee wa kiume ambalo linapendelea na kuhimiza mabadiliko kuhusu jambo hili. Hali kadhalika, wako wazee wa kike wanaotaka ukale udumishwe. Wazee hao wanajitokeza kama kikwazo kwa mapambano ya kutetea uhuru na haki kwa wanawake.

Wahusika vijana nao wanajitokeza kama watetezi wa haki za wanawake. Hata hivyo, wapo wachache wambao mtazamo wao kuhusu suala la wanawake unatetereka. Hao ni vijana wa kiume. Sababu wanazotoa kwa kutounga mkono mapambano hayo kikamilifu ni kuwa, wanachelea kulaumiwa na jamii kwa kutotii mila.

Vijana wote wa kike, wameonyesha hamu kubwa ya kuwa katika mstari wa mbele kupigana vita hivi. Hata ingawa juhudi zao zimekuwa zikikabiliwa na changamoto

kadha wa kadha, ari yao haikuonyesha kusita. Kwa hivyo, vijana wa kike na baadhi ya wazee wa kiume wanatupa matumaini kuwa ukombozi wa wanawake umewadia. Kama wahakiki wa kazi hizi tatu, tunahisi kuwa makundi haya mawili yanayopendelea mabadiliko yanawakilisha mitazamo ya wasanii wa kazi hizi.

Kwa mujibu wa utafiti huu, wazee wote wanaelekea kukubaliana kuwa mila na tamaduni za kale zinahitaji kudumishwa. Kwa hivyo, wazee wamejidhihirisha kama watetezi wa ukale ambao unaopingana na usasa unaowakilishwa na vijana. Kwa sababu hii, basi makisio yetu ya awali kuwa vijana ni wengi, wamesoma na ndio wanaokumbatia fikira za kimapinduzi na kimaendeleo ni ya kweli.

Madhumuni ya kwanza ya utafiti huu yalikuwa ni kutathmini nafasi ya vijana katika ukombozi wa mwanamke. Ni ukweli kuwa waandishi wa tamthilia hizi tatu wamewasawiri wahusika vijana kama msingi wa ukombozi wa mwanamke. Pia, tungependa kusisitiza hapa kuwa ni vijana wa kike tu ambao wanadhihirisha kujitolea kwao kushiriki katika mapambano hayo. Juhudi zao zinaungwa mkono na baadhi ya wazee wa kiume na vijana wachache wa kiume. Hili linamaanisha kuwa baadhi ya wanawake wazee na vijana wa kiume wachache ndio wanaochelewesha ukombozi wa mwanamke.

Madhumuni ya pili ya utafiti huu yalihusu kuchunguza juhudi zinazofanywa na wazee kuwatetea wanawake dhidi ya asasi za jamii zinazowakandamiza. Utafiti huu umetambua asasi mbili muhimu ambazo hutumiwa na jamii kumkandamiza mwanamke. Asasi hizo ni utamaduni na ndoa. Imedhihirika kwamba wanawake wazee wanatetea na kuhimiza kudumishwa kwa mila kandamizi. Kwa hivyo, badala ya wazee hao kuwapigania wanawake wenzao wanashiriki kuwakandamiza na vile vile kuchelewesha ukombozi wao. Pamoja na hayo, wapo wahusika wazee wachache wa kiume wanaodhihirisha nia yao ya kuwapigania wanawake. Wazee

hao ni kama vile Bw. Nia, Hamisi na Mzee Palipali. Wote hawa ni kielelezo cha wazee wa kiume wenye mawazo ya kimapinduzi.

Tunakisia kuwa mtazamo wa wazee hao ndio mtazamo wa waandishi wa tamthilia hizi tatu. Yamkini nia ya waandishi hawa ni kutuchorea picha ya baadhi ya wazee wakiume wenye mtazamo tofauti na wenzao wa kike kama mbinu ya kuikejeli jamii ya wanawake wanaopinga juhudi za wenzao kujikomboa. Hata hivyo, hatuna nia ya kuonyesha kuwa wanawake wote wazee tuliokutana nao katika utafiti huu wana mtazamo sawa kuhusu suala hili. Wapo wachache ambao ni kielelezo chema kwa vijana wote wanaopigania kuwe na mapinduzi juu ya suala hili.

Madhumuni ya tatu katika uchunguzi huu yalinuiwa kubainisha jinsi mwanamke anavyokandamizwa na vile vile kufichua baadhi ya changamoto zinazozikabili juhudi za kumkomboa. Utafiti huu umebainisha namna mbalimbali ambavyo wanawake hukandamizwa katika jamii. Ndoa na utamaduni zimetambulika kama taasisi zinazotumiwa na jamii kuwadhulumu wanawake. Kwa kiasi fulani dini imetajwa kama kisingizio kinachotumiwa na baadhi ya wanaume kuhalalisha udhalimu wao dhidi ya wanawake.

Katika ndoa mwanamke anatarajiwa kuchukua nafasi ya pili baada ya mwanamume. Maisha ya ndoa yanamhitaji mwanamume awe kiongozi wa nyumba na mwanamke awe mfuasi. Mawazo haya pia yanaungwa mkono na dini ambayo husisitiza kuwa mwanamke aliumbwa kutokana na ubavu wa mwanamume. Jambo hili linawafanya wanaume kujinaki kuwa wao ni viumbe bora kuliko wanawake. Hiki ndicho chanzo cha wanaume kuwadhulumu wanawake katika jamii nyingi ulimwenguni.

Madhila yanayowakumba wanawake ni mengi kama vile kupigwa, kutukanwa na kudharauliwa na waume zao ni mambo ya kawaida katika ndoa. Mwanamke

huanza kudhalilishwa angali msichana kupitia tamaduni zisizo na maana. Kwa mfano msichana haruhusiwi na mila kutangamana na wavulana wa rika lake kwa hofu kuwa ataharibiwa nao. Vile vile, wazazi wake hupenda kumchagulia mchumba bila hiari pamoja na kuhakikisha kuwa ndoa yake haitegemei mapenzi bali utajiri wa mume aliyechaguliwa. Kutokana na hali hii wanawake huishia kudhibitiwa na kutumikishwa kazi za nyumbani.

Pamoja na vitendo hivi vya kidhalimu pia wanawake hudhulumiwa kimapenzi pasipo kujali hisia zao. Wengine hulazimishwa kutii mila zinazomtaka mwanamke kuolewa kama mke wa pili baada ya kifo cha mumewe. kwa hivyo, ni dhahiri kuwa wanawake hukandamizwa kwa namna mbalimbali kwa mujibu wa kazi tulizozichunguza.

Wanawake wametambua elimu kama nguzo muhimu kufikia ukombozi wao lakini utafiti huu umetuonyesha kuwa baadhi ya wanawake wamenyimwa nafasi ya kupata elimu. Kutokana na sababu hii, viongozi wengi wa vyama vya wanawake hawana elimu ya kutosha kuwawezesha kuwaongoza wenzao vizuri. Jambo hili linatatiza juhudi za wanawake kujikomboa.

Umasikini ni tatizo lingine linalowakumba wanawake wengi katika jamii. Ili kujinua kiuchumi wanawake wameamua kuanzisha miradi ya kujipatia mapato. Hata hivyo, juhudi zao za kuanzisha vitega uchumi hukabiliwa na ukosefu wa mtaji. Ukosefu wa ufadhili na upungufu wa uwezo wa kupata mikopo ya benki huwa kizuizi kwa wanawake kujikwamua kiuchumi.

Tamaduni zinazopendelea maslahi ya mwanamume ni changamoto nyingine inayozikumba juhudi za wanawake kujikomboa. Mfumo wa jamii unaowataka wanawake kufuata baadhi ya mila zinazowadunisha ni kikwazo kikubwa. Mila zinamtaka mwanamke abakie nyumbani na asijaribu kujiingiza katika siasa. Vile

vile, tamaduni zingine zinawaruhusu wazazi kuwachagulia binti zao wachumba wasiowapenda au kuozwa mapema. Tamaduni hizo ni pamoja na zile zinazowaruhusu wanaume kuwarithi wajane. Mambo haya na mengine mengi tuliyoyajadili kwingineko katika utafiti huu husababisha changamoto kwa juhudi za wanawake kujikomboa.

Katika utafiti wetu tulinuia kuchunguza ushahidi kuhusu maswali matatu muhimu. Kwanza, tumejiuliza: Je, mtazamo wa vijana na wazee kuhusu ukombozi wa mwanamke unahitilafiana katika tamthilia zilizoshughulikiwa? Utafiti huu umebainisha kuwa madai ya nadharia hii tete yana ukweli. Tumegundua kuwa wazee wana mtazamo unaopingana na wa vijana juu ya suala hili. Ingawa si wazee wote walio na mtazamo huu kuhusu ukombozi wa wanawake, idadi kubwa ya wazee inaelekea kukubaliana kwa kauli moja kuwa lazima mila za kale zilindwe. Wazee tuliokutana nao katika uchunguzi huu hawapendelei kuwe na mabadiliko yoyote kuhusu hadhi na uhuru wa mwanamke katika jamii. Msimamo wao unapingana na wa vijana ambao wanapigania mabadiliko ya mila zinazowadunisha na kuwakandamiza wanawake. Kwa hivyo, tunaweza kudai kuwa wazee wamesawiriwa kama kielelezo cha uhafidhina nao vijana kama wanamapinduzi.

Swali letu la pili tulilojiuliza ni: Je, waandishi wa kazi hizi tatu wamewasawiri wahusika vijana kama msingi wa utetezi wa ukombozi wa mwanamke? Kulingana na matokeo ya utafiti wetu imedhihirika kuwa makisio ya nadharia tete yetu ya pili ni ya kweli. Kama tulivyokwisha kuonyesha kwingineko katika uhakiki huu, vijana hasa wale wa kike wameonyesha juhudi kubwa kupinga udhalimu dhidi yao na wanawake wote kwa jumla. Kwa hivyo, ingawa vijana wameshirikiana na wahusika wengine wazee kutetea maslahi ya wanawake, tumetambua kujitolea kwingi kwa vijana katika vita hivi kuliko wahusika wengine. Hilo ni thibitisho kuwa vijana wametumiwa na waandishi kama msingi wa utetezi wa ukombozi wa mwanamke.

Swali letu la tatu tulilonuia kulijibu ni: Je, waandishi wa tamthilia hizi tatu wametambua kuwa mwanamke anadhulumiwa na anahitaji ukombozi?. Jibu la swali hili ni ndio. Utafiti huu umeibua namna mbalimbali ambavyo wanawake hudhulumiwa katika jamii inayoendeshwa kwa hatamu za mwanamume. Aidha, kuna ushahidi kwamba juhudi nyingi zinafanywa ili kumkomboa mwanamke kutokana na hali hiyo. Isitoshe,waandishi wenyewe wameonyesha kutambua tatizo la wanawake na wanaelekea kulipa umuhimu mkubwa katika kazi zao. Jambo hili limethibitishwa na namna walivyowasawiri wahusika wengi wenye nia na ari ya kupigania ukombozi wa mwanamke.

## 5.2 Tafiti za baadaye

Utafiti huu ni wa kifasihi na umejikita katika utanzu wa drama. Fasihi ina tanzu zingine mbili muhimu ambazo ni ushairi na riwaya. Kwa hivyo, tunapendekeza tafiti za baadaye zilenge kubainisha mitazamo ya vijana na wazee katika riwaya, hadithi fupi na ushairi. Vile vile, watafiti wa baadaye wanaweza kuhusisha ulinganishaji wa mitazamo ya vijana na wazee kwa mujibu wa kazi zilizoandikwa na wasanii wa jinsia tofauti.

## 5.3 MAREJELEO


Bible Society of Kenya, (1997) *The Holy Bible in Kiswahili.* Nairobi.

De Beauviore, S. (1949) *The Second Sex.* London: Pan books Publishers.

Dhahabu, L. (1994) 'Uumbaji na uendelezaji wa wahusika katika tamthilia nne za Penina Muhando' Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu cha Nairobi (haijachapishwa).

Gachukia, E. (1993) *Empowering Kenya women.* Nairobi: National committee on the status of women. (Makala ambayo hayajachapishwa bado).

Hussein, E. (1971) *Wakati ukuta.* Nairobi: East African Publishing House.

Kabira, W. / Nzioki, E. (1993) *Celebrating Women's Resistance.* Nairobi: African's woman's perspectives.

*Kamusi ya Kiswahili sanifu* (2004). Oxford University Press. Nairobi.

Katola, E. (2006) " Udhalimu dhidi ya wahusika wa kike katika tamthilia za Kiswahili" , Tasnifu ya MA: Chuo Kikuu cha Nairobi (haijachapishwa bado).

Katini, A.K. (2003) *Mama Ee.* Nairobi: East Africa Educational Publishers.

Kiango, S. (1997) "Taswira ya mwanamke katika tamthilia za Kiswahili za Kenya". Tasnifu ya MA: Chuo kikuu cha Nairobi (haijachapishwa bado).

Lugano, R. (1989) "Mwanamke katika riwaya za Kezilahabi". Tasnifu ya MA: Chuo Kikuu cha Nairobi (haijachapishwa bado).

Mazrui, A. (1982) *Kilio cha Haki*. Nairobi: Longman.

Mbatiah, M. (2001) *Kamusi ya fasihi na nadharia*. Nairobi: Standard Textbooks Graphics and Publishing.

________ (2006) *Migogoro*. Nairobi: The JomoKenyatta Foundation.

Mbughuni, P. (1982) "The image of woman in Kiswahili prose fiction" *Kiswahili, Juzuu 49/*. uk 24.

Mohamed, S. (2000) *Kitumbua kimeingia mchanga*. Nairobi: Oxford University Press.

Momanyi, C. (2002) "Swala la uana katika fasihi ya kiswahili" katika Inyani Simala (Mhariri) Utafiti wa Kiswahili, uk. 61-69

Ndungo, C. (1985) " Wanawake na mabadiliko ya kihistoria katika Kiswahili". Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu cha Nairobi (haijachapishwa bado).

Njogu, K./
Chimera, R.(1999) *Ufundishaji wa fasihi Nadharia na mbinu*. Nairobi: JomoKenyetta Foundation.

Nyamberi, H.(1997) "Mwamko wa mwanamke katika tamthilia za Penina Muhado". Tasnifu ya MA: Chuo kikuu cha Nairobi (haijachapishwa ).

Nyerges, A. (1962) *Women in Hungary*. Budapest: University Printing House.

Ozkaya, G. (1981) *From Captivity to Freedom: Woman's fight*. Ankara: T.W.A Publications.

Palmer, P. (1989) *Contempory Women's Fiction: Narrative practice and Feminist theory*. New York: Harvester wheatsheaf.

Tuki (2000) *English - Swahili dictionary 2nd edition*. Dares salaam.

Wa Mberia, K. (1997) *Natala*. Nairobi: Marimba publications Ltd.

Wamitila, K. / Mbuthia, E. (2003) Mwongozo *wa kitumbua kimeingia mchanga*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Wamitila, K. (2003) Kamusi *ya fasihi, Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Books.

________________, (2004) *Kichocheo cha fasihi: Simulizi na andishi*. Nairobi: Focus books.

Wolgast, E. (1980) *Equality and the rights of women*. Ithaca and London: University Press.

Wollstonecraft, M. (1792) A *Vindication of the rights of women*. Harmondworths: Penguin (chapa ya kwanza 1792), BlackWell Publishers.